**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

# TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI 2021 HADI JUNI 2022 KWA AJILI YA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI UTAKAOFANYIKA TAREHE 05.08.2022

*Imeandaliwa na;*

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji

S.L.P 73

**TUNDUMA -SONGWE**

## YALIYOMO


1. Dibaji ………………………………………………….. Uk. 3-4
2. Taarifa ya mapato na matumizi………………………………………………. Uk.4-22
3. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo……………………………... Uk.23-27
4. Taarifa za Divisheni na Vitengo
    i. Maendeleo ya Jamii ……………………………………………………Uk.27-29
    ii. Uwekezaji,Viwanda na Biashara……………………………………….Uk.29-30
    iii. Miundombinu,Maendeleo Vijijini na Mijini ……………………………..Uk.31-34
    iv. Elimu ya Awali na Msingi………………………………………………..Uk.34
    v. Elimu Sekondari…………………………………………………………Uk.35-36
    vi. Utawala na Usimamizi wa Raslimali Watu………………………………Uk.36-38
    vii. Seksheni ya Ardhi na Mipangomiji………………………………………. Uk.39-41
    viii. Kilimo,Mifugo na Uvuvi…………………………………………………Uk.41-42
    ix. Huduma za Kisheria……………………………………………………Uk.43
    x. Udhibiti wa Taka na Usafi wa Mazingira…………………………………Uk.44-49
    xi. Afya,Ustawi wa Jamii na Huduma za Lishe……………………………..Uk.50-52
5. Taarifa ya utekelezaji wa zoezi la Anwani za Makazi na Postikodi……….. Uk.52-57
6. Taarifa Maandalizi ya Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru 2022………………... Uk.57
7. Hitimisho………………………………………………………………………Uk.58

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

**05.08.2022**

Mhe.Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Tunduma

Mhe.Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji

Waheshimiwa Wabunge

Katibu Tawala Mkoa wa Songwe

Kamati ya Usalama Wilaya ya Momba

Waheshimiwa Madiwani

Wageni Waalikwa

Waandishi wa Habari

Watumishi wa Halmashauri ya Mji

Wananchi wote mliohudhuria

**KUH: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI 2021 HADI JUNI 2022 KWA AJILI YA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 05.08.2022**

## 1.0 Utangulizi.

Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!!!

Ninawakaribisha katika mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Tunduma ambalo pamoja na mambo mengine litapokea taarifa ya utekelezaji kwa mwaka unaoishia tarehe **30** Juni **2022.**

Kipekee ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana siku ya leo tukiwa na bukheri wa afya njema.

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji Tunduma imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kuzingatia miongozo na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka **2021/2022** ikijikita kwenye vipaumbele vitatu (3) ambavyo ni;-

Ukusanyaji wa mapato,Usafi wa Mazingira na Utawala na Utawala Bora.

Aidha katika kutekeleza misingi tuliyojiwekea kwa kuzingatia vipaumbele pamoja na uwepo wa changamoto tumeweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa na kutimiza baadhi ya matarajio ya wananchi wa Mji wa Tunduma katika utoaji wa huduma bora za kijamii katika Sekta ya Elimu,Afya na huduma za kiuchumi kama vile Barabara,Masoko,Biashara na Viwanda,Kilimo,Ufugaji,Mipangomiji na Usafi wa Mazingira ambapo Halmashauri yetu ni miongoni mwa Halmashauri zinazofanya vizuri Kitaifa katika Nyanja mbalimbali kama ifuatavyo;-

**MAPATO:**

**Mhe.Mwenyekiti,**

Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Mji wa Tunduma imeidhinishiwa makisio ya kukusanya mapato ya ndani na kupokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani mbalimbali wa Maendeleo Jumla ya **TZS. 31,644,378,303.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali kama inavyoonekana kwenye Jedwali lifuatalo:-

**JEDWALI NA. 1: MUHTASARI WA MAKISIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

| NA. | MAELEZO | KIASI (TSHS) |
|---|---|---|
| I | Fedha za makusanyo ya mapato ya ndani | 5,635,690,500.00 |
| II | Fedha za ruzuku ya serikali kwa ajili ya Matumizi mengineyo | 792,117,455.00 |
| III | Fedha za ruzuku ya Miradi ya Maendeleo na wa Wahisani | 12,781,853,000.00 |
| IV | Fedha za ruzuku kwa ajili ya Mishahara | 12,434,717,348.00 |
| | **JUMLA KUU YA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022** | **31,644,378,303.00** |

Aidha, baada ya kufanya vizuri katika makusanyo ya mapato ya ndani kwa kipindi cha robo ya pili ya Mwaka wa fedha **2021/2022** Kamati ya Fedha na Utawala iliidhinisha mapendekezo ya Menejimenti ya kuongeza bajeti ya mapato ya ndani kwa kiasi cha **TZS. 2,0000,000.00** Hivyo kufanya bajeti ya makusanyo ya mapato ndani kuongezeka kutoka bajeti ya awali ya **TZS. 5,635,690,500** hadi kufikia **TZS. 7,635,690,500.00** na kufanya bajeti kuu ya makusanyo ya mapato ya ndani na mapokezi ya fedha kutoka Serikali Kuu kuongezeka kutoka **TZS. 31,644,378,303.00** hadi **TZS.33,644,378,303.00**

**Mhe:Mwenyekiti,**

Kwa kipindi cha mwezi Juni,2022 Halmashauri imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani na kupokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani kiasi cha **TZS.2,111,588,309** na kufanya Jumla ya mapato tuliyokusanya na kupokea kuanzia Mwezi Julai,**2021** hadi Juni,**2022** kufikia **TZS 31,840,979,394** ambayo ni sawa na **asilimia 94.5** ya makisio ya mapato kwa mwaka wa fedha **2021/2022.**

**JEDWALI NA.2: MUHTASARI WA MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI NA MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU YA SERIKALI KUU NA WAHISANI WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI 2022**

| MAELEZO | MAKISIO YA MWAKA WA FEDHA 2021/22 | MAPATO TULIYOKUSANYA KUANZIA JULAI-MEI,2022 | MAPATO TULIYOKUSANYA KWA MWEZI JUNI,2022 | MAPATO TULIYOKUSANYA KUANZIA JULAI-JUNI,2022 | TOFAUTI KATI YA MAKISO NA MAKUSANYO | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Fedha za makusanyo ya Mapato ya ndani | 7,635,690,500.00 | 7,732,545,664.30 | 861,852,209.00 | 8,594,397,873.30 | -958,707,373.30 | 113 |
| Fedha za Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 792,117,455.00 | 739,136,788.38 | 56,472,165.28 | 795,608,953.66 | -3,491,498.66 | 100 |
| Fedha za Ruzuku kwa ajili ya Mishahara (PE) | 12,434,717,348.00 | 10,157,522,150.00 | 887,497,000.00 | 11,045,019,150.00 | 1,389,698,198.00 | 89 |
| Fedha za Ruzuku za | 12,781,853,000.00 | 11,100,186,482.04 | 305,766,934.98 | 11,405,953,417.02 | 1,375,899,582.98 | 89 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Miradi ya Maendeleo | | | | | | |
| **JUMLA KUU** | **33,644,378,303.00** | **29,729,391,084.72** | **2,111,588,309.26** | **31,840,979,393.98** | **1,803,398,909.02** | **95** |

**Mhe:Mwenyekiti**,

Katika kipindi cha Mwezi Juni,2022 Halmashauri ilipokea fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani wa Maendeleo kiasi cha **TZS. 1,100,112,034.28** kwa ajili ya ulipaji wa Mishahara ya watumishi wa Ruzuku,Elimu Bila Malipo na Miradi Maendeleo kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini:-

**JEDWALI NA:3 MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI,2022**

| S/NA | MAELEZO YA FEDHA | FEDHA |
|---|---|---|
| i | Mishahara ya watumishi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa Mwezi Juni,2022 | 887,497,000.00 |
| ii | Ruzuku ya matumizi ya kawaida (Other charges) | 56,472,165.28 |
| iii | Fedha za mfuko wa Afya(Basket Fund) | 75,591,912.00 |
| iv | Fedha za usimamizi wa miradi ya UVIKO 19 | 9,250,000.00 |
| v | Elimu bila malipo | 220,925,022.98 |
| | **JUMLA KUU TZS.** | **1,249,736,100.26** |

**MATUMIZI:**

**Mhe:Mwenyekiti,**

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikasimia kutumia kiasi cha **TZS.31,644,378,303** kutoka katika vyanzo mbalimbali, Aidha kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilibakiwa na bakaa kiasi cha **TZS.112,042,729.95** Fedha hizi zilizosalia zimeunganishwa kwenye makisio ya matumizi ya mwaka huu wa fedha ili ziweze kutumika hivyo kufanya makisio ya Matumizi kuongezeka kutoka **TZS. 31,644,378,303.00** Hadi kufikia kiasi cha **TZS.31,756,421,032.95**. Aidha, Baada ya kufanya vizuri kwenye makusanyo ya mapato ya ndani Kamati ya Fedha na Utawala iliridhia Mapendekezo ya Menejimenti ya kuongeza bajeti ya Matumizi ya Mapato ya ndani kwa kiasi cha **TZS. 2,000,000,000** Hivyo kufanya bajeti kuu ya matumizi kuongezeka kutoka **TZS. 31,756,421,032.95** hadi kufikia **TZS. 33,756,421,032.95**

**JEDWALI NA. 5 :MUHTASARI WA SURA YA MATUMIZI YA MWAKA 2021/2022**

| MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 |
|---|---|
| Salio Anzia la mwaka 2020/2021 | 112,042,729.95 |
| Makusanyo ya vyanzo vya ndani | 7,635,690,500.00 |
| Ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida (OC) | 792,117,455.00 |
| Ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya Mishahara | 12,434,717,348.00 |
| Fedha za Miradi ya Maendeleo na wahisani | 12,781,853,000.00 |
| **JUMLA KUU YA BAJETI YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022** | **33,756,421,032.95** |

**Mhe:Mwenyekiti,**

Kwa kipindi cha mwezi Juni,2022 Halmashauri imetumia kiasi cha **TZS. 5,345,171,319** na kufanya Jumla ya matumizi kuanzia **01.07.2021** hadi **31.06.2022** kufikia **TZS. 28,731,791,491** ikiwa ni sawa na **asilimia 85** ya makisio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kama Jedwali lifuatalo linavyoonekana:-

**JEDWALI NA. 6: MUHTASARI WA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA KUISHIA 30 JUNI2022**

| MAELEZO | MAKISIO YA MWAKA 2021//2022 | MATUMIZI KUANZIA JULAI HADI MEI,2022 | MATUMIZI HALISI MWEZI JUNI,2022 | MATUMIZI HALISI MWEZI JULAI HADI JUNI,2022 | TOFAUTI YA MAKISIO NA MATUMIZI | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bakaa | 112,042,729.95 | 100,602,880.00 | 11,439,850.00 | 112,042,730.00 | -0.05 | 100 |
| Matumizi ya kawaida kwa Fedha za Mapato ya Ndani | 3,313,687,279.80 | 3,051,773,284.13 | 268,100,538.00 | 3,319,873,822.13 | -6,186,542.33 | 100 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Miradi ya Maendeleo kwa Fedha za Mapato ya Ndani | 4,322,003,220.00 | 3,145,263,298.00 | 1,977,728,646.00 | 5,122,991,944.00 | -800,988,724.00 | 119 |
| Ruzuku ya Matumizi ya kawaida (OC) | 792,117,455.00 | 716,048,315.35 | 78,865,099.00 | 794,913,414.35 | -2,795,959.35 | 100 |
| Ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya Mishahara | 12,434,717,348.00 | 10,158,011,150.00 | 887,497,000.00 | 11,045,508,150.00 | 1,389,209,198.00 | 89 |
| Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo na wahisani | 12,781,853,000.00 | 6,214,921,244.50 | 2,122,029,185.60 | 8,336,950,430.10 | 4,444,902,569.90 | 65 |
| **JUMLA KUU** | **33,756,421,032.75** | **23,386,620,171.98** | **5,345,660,318.60** | **28,732,280,490.58** | **5,024,140,542.17** | **85** |

**MAKUSANYO YA MAPATO KUANZIA 01.07.2021 HADI 30.06.2022**

| IDARA | MAELEZO YA KASMA/CHANZO | MAKISIO 2021/22 | Jumla ya Mapato kuanzia 01.07.2021 Hadi 31.05.2022 | Mapato ya Mwezi Juni ( 01 hadi 30.06.2022) | Jumla ya Mapato kuanzia 01.07.2021 Hadi 30.06.2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi | Ada vibali vya ujenzi | 21,000,000.00 | 20,250,000.00 | 3,730,000.00 | 23,980,000.00 | 114 |
| | Ada ya ukaguzi wa michoro | 4,200,000.00 | 4,064,000.00 | 733,000.00 | 4,797,000.00 | 114 |
| | Ushuru wa Madini ya Ujenzi (mchanga, kokoto na mawe) | 45,625,000.00 | 23,307,000.00 | 2,852,000.00 | 26,159,000.00 | 57 |
| | Mapato yatokanayo na Uuzaji wa Tofali | 500,000,000.00 | 708,878,600.00 | 64,200,000.00 | 773,078,600.00 | 155 |
| | **Jumla Ndogo** | **570,825,000.00** | **756,499,600.00** | **71,515,000.00** | **828,014,600.00** | **145** |
| **Elimu Msingi - Utamaduni** | Mchango Usafi wa mazingira Chekechea | 1,120,000.00 | 300,000.00 | | 300,000.00 | 27 |
| | Matangazo ya biashara | 10,400,000.00 | 10,485,000.00 | 1,450,000.00 | 11,935,000.00 | 115 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ada ya kumbi za starehe na michezo | 3,000,000.00 | 2,241,250.00 | 60,000.00 | 2,301,250.00 | 77 |
| | **Jumla Ndogo** | 14,520,000.00 | 13,026,250.00 | 1,510,000.00 | 14,536,250.00 | 100 |
| **Afya** | Ada ya upimaji Afya (medical examination) | 10,000,000.00 | 11,524,000.00 | 535,000.00 | 12,059,000.00 | 121 |
| | Mapato yatokanayo na Duka la dawa | | 12,288,614.00 | 255,880.00 | 12,544,494.00 | |
| | **Jumla Ndogo** | **10,000,000.00** | **23,812,614.00** | **790,880.00** | **24,603,494.00** | 246 |
| **Ardhi** | Mapato ya ardhi | 5,000,000.00 | 1,680,987.00 | 5,852,000.00 | 7,532,987.00 | 151 |
| | Ada ya kupanga na kupima | 10,500,000.00 | 3,634,432.00 | 60,000.00 | 3,694,432.00 | 35 |
| | Ukodishaji wa RTK | 500,000.00 | - | | - | - |
| | **Jumla Ndogo** | **16,000,000.00** | **5,315,419.00** | **5,912,000.00** | **11,227,419.00** | 70 |
| **Maliasili** | Maombi ya kusafisha mashamba mapya | 2,500,000.00 | - | | - | - |
| | Ushuru wa Mazao ya | 30,000, | 26,447,000.00 | 2,635,000.00 | 29,082,000.00 | 97 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | misitu | 000.00 | | | | |
| | Kibali cha kubeba kuni | 7,500,000.00 | 8,576,200.00 | | 8,576,200.00 | 114 |
| | Ushuru wa mirunda/milingoti | 25,000,000.00 | 44,579,000.00 | 4,236,000.00 | 48,815,000.00 | 195 |
| | Ushuru wa mazao ya nyuki | 5,000,000.00 | 2,832,700.00 | | 2,832,700.00 | 57 |
| | **Jumla Ndogo** | **70,000,000.00** | **82,434,900.00** | **6,871,000.00** | **89,305,900.00** | 128 |
| **Mifugo** | Ada ya machinjio ng'ombe | 63,875,000.00 | 54,799,000.00 | 4,710,000.00 | 59,509,000.00 | 93 |
| | Ada ya machinjio mbuzi na kondoo | 19,440,000.00 | 18,498,000.00 | 1,659,000.00 | 20,157,000.00 | 104 |
| | Nguruwe | 16,200,000.00 | 6,840,000.00 | 774,000.00 | 7,614,000.00 | 47 |
| | Vibali vya usafirishaji wa ngozi/Mifugo | 1,800,000.00 | 940,000.00 | | 940,000.00 | 52 |
| | Ushuru wa samaki na dagaa | 120,000,000.00 | 114,949,000.00 | 7,744,500.00 | 122,693,500.00 | 102 |
| | Leseni ya maduka ya mazao ya uvuvi(samaki) | 1,200,000.00 | 1,680,000.00 | 30,000.00 | 1,710,000.00 | 143 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mnada wa mifugo (Chiwezi) | 1,050,000.00 | 2,000,200.00 | | 2,000,200.00 | 190 |
| | Faini za Mifugo | 1,000,000.00 | 550,000.00 | | 550,000.00 | 55 |
| | **Jumla Ndogo** | **224,565,000.00** | **200,256,200.00** | **14,917,500.00** | **215,173,700.00** | 96 |
| **Mazingira (Afya kinga)** | Ushuru wa usafi wa Mazingira majengo ya biashara | 151,500,000.00 | 161,921,090.00 | 27,470,840.00 | 189,391,930.00 | 125 |
| | Ushuru wa usafi wa Mazingira sehemu za biashara(Soko la majengo) | 42,050,000.00 | 5,587,400.00 | 578,600.00 | 6,166,000.00 | 15 |
| | Ushuru wa usafi wa Mazingira 20% makusanyo ya kata | 24,000,000.00 | 42,038,980.00 | 3,543,300.00 | 45,582,280.00 | 190 |
| | Kushusha na kupakia | 180,000,000.00 | 97,211,560.00 | 11,195,000.00 | 108,406,560.00 | 60 |
| | choo cha soko kuu | 20,900,000.00 | 23,185,200.00 | 1,746,400.00 | 24,931,600.00 | 119 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | choo cha soko la mazao | 3,960,000.00 | 6,289,000.00 | 597,200.00 | 6,886,200.00 | 174 |
| | Choo cha Stendi kuu | 3,600,000.00 | 4,300,000.00 | | 4,300,000.00 | 119 |
| | Choo cha Tazara | | 5,177,200.00 | 1,119,000.00 | 6,296,200.00 | |
| | Choo cha soko la majengo | 5,400,000.00 | 6,580,000.00 | 532,000.00 | 7,112,000.00 | 132 |
| | **Jumla Ndogo** | **431,410,000.00** | **352,290,430.00** | **46,782,340.00** | **399,072,770.00** | 93 |
| **Utawala** | **Ushuru wa usafi wa mazingira Custom** | | | | | |
| | Ushuru wa magari madogo (IT) | 236,875,000.00 | 282,600,000.00 | 23,985,000.00 | 306,585,000.00 | 129 |
| | Ushuru wa magari makubwa (track) | 1,230,000,000.00 | 1,331,097,000.00 | 115,740,000.00 | 1,446,837,000.00 | 118 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,466,875,000.00** | **1,613,697,000.00** | **139,725,000.00** | **1,753,422,000.00** | 120 |
| | Mapato ya container yaliyowekwa | 1,200,000.00 | 1,650,000.00 | | 1,650,000.00 | 138 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri | | | | | |
| | **vibanda vya Halmashauri** | | | | | |
| | Soko la Tazara | 97,680,000.00 | - | | - | - |
| | Soko kuu | 311,400,000.00 | 219,292,000.92 | 60,440,000.00 | 279,732,000.92 | 90 |
| | Makambini | 600,000.00 | 350,000.00 | 25,000.00 | 375,000.00 | 63 |
| | Soko la Mazao | 20,160,000.00 | 17,989,800.00 | 550,000.00 | 18,539,800.00 | 92 |
| | Soko la Standi | 24,000,000.00 | 23,500,000.00 | | 23,500,000.00 | 98 |
| | Soko la mpemba | 1,800,000.00 | 745,000.00 | 40,000.00 | 785,000.00 | 44 |
| | Ada ya baraza ya kata | 300,000.00 | 14,000.00 | | 14,000.00 | 5 |
| | Pango la Mnara wa simu (s/m Tunduma) | 6,600,000.00 | 6,600,000.00 | | 6,600,000.00 | 100 |
| | Ushuru wa Huduma- | 26,000, | 42,127,192.74 | | 42,127,192.74 | 162 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Minara ya Simu | 000.00 | | | | |
| | **Jumla Ndogo** | **489,740,000.00** | **312,267,993.66** | **61,055,000.00** | **373,322,993.66** | 76 |
| **Fedha na Biashara** | Leseni za biashara | 320,000,000.00 | 372,401,478.92 | 22,494,000.00 | 394,895,478.92 | 123 |
| | Leseni za vileo | 12,600,000.00 | 21,061,300.22 | 1,881,700.00 | 22,943,000.22 | 182 |
| | Ushuru wa huduma (Service Levy) | 259,500,000.00 | 452,213,851.03 | 38,894,276.00 | 491,108,127.03 | 189 |
| | Parking binafsi (YARD) | 46,537,500.00 | 46,956,000.00 | 980,000.00 | 47,936,000.00 | 103 |
| | Parking ya Halmashauri(Yard-Chapwa) | 32,850,000.00 | 52,098,000.00 | 6,522,000.00 | 58,620,000.00 | 178 |
| | Ushuru wa stend | 146,000,000.00 | 161,181,000.00 | 14,629,000.00 | 175,810,000.00 | 120 |
| | Ushuru wa malazi (Hotel Levy) | 120,000,000.00 | 190,722,070.00 | 21,131,700.00 | 211,853,770.00 | 177 |
| | Ushuru wa magulio | 1,300,000.00 | 1,000,400.00 | 142,900.00 | 1,143,300.00 | 88 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Faini Mbalimbali | 40,000,000.00 | 61,836,200.00 | 3,818,000.00 | 65,654,200.00 | 164 |
| | Mapato Mengineyo | 2,893,000.00 | 11,641,840.00 | 15,383.00 | 11,657,223.00 | 403 |
| | **Ada ya usajili wa Bajaji, Pikipiki,Taxi na daladala** | | | | | |
| | Bajaji | 25,000,000.00 | 24,056,000.00 | | 24,056,000.00 | 96 |
| | Pikipiki | 14,000,000.00 | 18,510,000.00 | | 18,510,000.00 | 132 |
| | Taxi | 600,000.00 | 400,000.00 | | 400,000.00 | 67 |
| | Usajili wa magari mengine ya biashara | 2,000,000.00 | 1,430,000.00 | | 1,430,000.00 | 72 |
| | Usajili wa daladala | 500,000.00 | - | | - | - |
| | **Jumla Ndogo** | **1,023,780,500.00** | **1,415,508,140.17** | **110,508,959.00** | **1,526,017,099.17** | 149 |
| **Ugavi** | Ada ya Maombi ya zabuni | 500,000.00 | 1,340,000.00 | | 1,340,000.00 | 268 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **-** | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **500,000.00** | **1,340,000.00** | | **1,340,000.00** | 268 |
| **Kilimo** | **Ushuru wa mazao** | | | | | |
| | Ushuru wa mahindi | 1,300,000,000.00 | 966,301,925.00 | 207,379,600.00 | 1,173,681,525.00 | 90 |
| | Ushuru wa Maharage | 130,000,000.00 | 221,062,000.00 | 9,924,000.00 | 230,986,000.00 | 178 |
| | Ushuru wa vitunguu na mbogamboga | 115,500,000.00 | 116,700,900.00 | 5,097,000.00 | 121,797,900.00 | 105 |
| | Ushuru wa mpunga na Mchele | 180,000,000.00 | 180,279,300.00 | 17,669,000.00 | 197,948,300.00 | 110 |
| | Ushuru wa Viazi,ulezi,ufuta, uwele alizeti,mtama na mazao mengineyo | 1,108,000,000.00 | 1,038,373,600.00 | 116,208,500.00 | 1,154,582,100.00 | 104 |
| | Faini za utoroshaji mazao | 20,000,000.00 | 21,124,400.00 | | 21,124,400.00 | 106 |
| | Ushuru wa Soko ( soko la Mazao) | 20,000,000.00 | 11,514,000.00 | 1,210,000.00 | 12,724,000.00 | 64 |
| | Ada ya upimaji Mizani | 27,375, | 13,459,800.00 | 1,010,000.00 | 14,469,800.00 | 53 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 000.00 | | | | | |
| | **Jumla Ndogo** | 2,900,875,000.00 | 2,568,815,925.00 | 358,498,100.00 | 2,927,314,025.00 | 101 | |
| **Maendeleo ya Jamii** | Usajili wa vikundi | 1,500,000.00 | - | | - | - | |
| | Ada ya vikundi | 1,500,000.00 | 10,000.00 | | 10,000.00 | 1 | |
| | **Jumla Ndogo** | 3,000,000.00 | 10,000.00 | - | 10,000.00 | 0 | |
| **Jumla ya makusanyo ownsource proper** | | | **7,222,090,500.00** | **7,345,274,471.83** | **818,085,779.00** | **8,163,360,250.83** | 1 1 3 |
| **B: MAPATO YA MICHANGO YA KIJAMII(USER FEE)** | | | | | | | |
| **Elimu** | **ADA ZA SHULE Elimu secondary** | | | | | | |
| | Mpemba secondary | 10,010,000.00 | 9,113,000.00 | 5,775,000.00 | 14,888,000.00 | 149 | |
| | Nyerere Secondary | 15,960,000.00 | 13,920,000.00 | 2,728,000.00 | 16,648,000.00 | 104 | |
| | **Jumla ya Ada Shule za Sekondary.** | **25,970,000.00** | **23,033,000.00** | **8,503,000.00** | **31,536,000.00** | 121 | |
| | **Elimu Msingi** | | | | | | |
| | English | | | 10,724,000.00 | | 135 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Medium | 60,750,000.00 | 71,275,980.92 | | 81,999,980.92 | |
| | **Jumla ya Ada Shule Msingi.** | **60,750,000.00** | **71,275,980.92** | **10,724,000.00** | **81,999,980.92** | 135 |
| | **Jumla kuu ya Ada za shule msingi na sekondary** | **86,720,000.00** | **94,308,980.92** | **19,227,000.00** | **113,535,980.92** | 131 |
| **Idara ya Afya (TIBA)** | **Uchangiaji wa papo kwa papo kituo cha afya** | | | | | |
| | Kituo cha Afya | 246,000,000.00 | 245,229,410.00 | 23,801,080.00 | 269,030,490.00 | 109 |
| | Zahanati ya Katete | 4,020,000.00 | 3,590,445.00 | 230,700.00 | 3,821,145.00 | 95 |
| | Zahanati ya chiwezi | 1,320,000.00 | 1,938,000.00 | 204,000.00 | 2,142,000.00 | 162 |
| | Zahanati ya Nandanga | 2,160,000.00 | 3,903,060.00 | 165,650.00 | 4,068,710.00 | 188 |
| | Zahanati ya Mpande | 300,000.00 | 495,000.00 | 45,000.00 | 540,000.00 | 180 |
| | Zahanati ya Makambini | 2,580,000.00 | 1,488,000.00 | 93,000.00 | 1,581,000.00 | 61 |
| | Hospitali ya wilaya | 48,000, | - | | - | - |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 000.00 | | | | |
| | Zahanati ya Tunduma(Custom) | 1,200,000.00 | 148,400.00 | | 148,400.00 | 12 |
| | **Jumla Ndogo Papo kwa Papo** | **305,580,000.00** | **256,792,315.00** | **24,539,430.00** | **281,331,745.00** | 92 |
| | **CHF (Community Health Fund)** | | | | | |
| | Kituo cha Afya | 6,000,000.00 | 12,900,131.55 | | 12,900,131.55 | 215 |
| | Zahanati ya Katete | 600,000.00 | - | | - | - |
| | Zahanati ya chiwezi | 300,000.00 | - | | - | - |
| | Zahanati ya Nandanga | 240,000.00 | - | | - | - |
| | Zahanati ya Mpande | 180,000.00 | - | | - | - |
| | Zahanati ya Makambini | 600,000.00 | - | | - | - |
| | **Jumla Ndogo CHF** | **7,920,000.00** | **12,900,131.55** | **-** | **12,900,131.55** | 163 |
| | | | | | | |
| | **NHIF(Nationa** | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **l Health Insuarance Fund)** | | | | | |
| | Kituo cha Afya | 12,000,000.00 | 22,490,880.00 | | 22,490,880.00 | 187 |
| | Zahanati ya Katete | 600,000.00 | 328,705.00 | | 328,705.00 | 55 |
| | Zahanati ya chiwezi | 60,000.00 | - | | - | - |
| | Zahanati ya Nandanga | 60,000.00 | 300,680.00 | | 300,680.00 | 501 |
| | Zahanati ya Mpande | 60,000.00 | - | | - | - |
| | Zahanati ya Makambini | 600,000.00 | 149,500.00 | | 149,500.00 | 25 |
| | **Jumla Ndogo NHIF** | **13,380,000.00** | **23,269,765.00** | **-** | **23,269,765.00** | 174 |
| | **Jumla Ndogo ya Michango ya Afya** | **326,880,000.00** | **292,962,211.55** | **24,539,430.00** | **317,501,641.55** | 97 |
| **Jumla ya makusanyo ya michango ya** | | **413,600,000.00** | **387,271,192.47** | **43,766,430.00** | **431,037,622.47** | 104 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kijamii | | | | | | |
| JUMLA KUU YA MAPATO YA NDANI(A + B) | | 7,635,690,500.00 | 7,732,545,664.30 | 861,852,209.00 | 8,594,397,873.30 | 113 |

- **TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KUISHIA TAREHE 30 JUNI 2022**

Katika mwaka wa fedha **2021/2022,** Halmashauri ya Mji wa Tunduma ilipanga kupokea na kutumia jumla ya Shs.**17,115,107,300.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka vyanzo mbalimbali kama Serikali Kuu, Wahisani na Mapato ya ndani, hadi kufikia mwezi Juni **2022**. Halmashauri imepokea jumla ya Sh. **19,583,343,600.04** sawa na asilimia **88** kutoka vyanzo mbalimbali. Halmashauri kwa bajeti yake ya Mapato ya ndani imetenga kiasi cha Tshs **4,333,254,300.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi cha Tshs. **4,398, 188, 982. 00** sawa na asilimia **101.4** ya mapato ya ndani kimepelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Mapato na matumizi ya fedha za miradi ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

**C MIRADI YA MAENDELEO INAYOTEKELEZWA KATIKA NGAZI YA HALMASHAURI - RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU NA WAHISANI**

| NA | MAELEZO | MAKISIO YA MWAKA 2021/2022 | JUMLA YA MAPOKEZI JULAI-MEI,2022 | MAPOKEZI KWA MWEZI JUNI 2022 | JUMLA YA MAPOKEZI JULAI-JUNI,2022 | JUMLA YA MATUMIZI HADI JUNI | TOFAUTI YA MAPATO NA MATUMIZI NA MAPOKEZI HALISI | (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MFUKO WA JIMBO | 35,000,000.00 | 35,000,000.00 | - | 35,000,000.00 | 35,000,000.00 | - | 100 |
| 2 | UJENZI WA JENGO LA UTAWALA | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 | - | 1,000,000,000.00 | 953,117,341.38 | 46,882,658.62 | 100 |
| 3 | UJENZI WA NYUMBA YA MKURUGENZI | 150,000,000.00 | 150,000,000.00 | - | 150,000,000.00 | 150,000,000.00 | - | 100 |
| 4 | MIRADI MIKAKATI - MAEGESHO YA MALORI | 400,000,000.00 | 400,000,000.00 | - | 400,000,000.00 | 382,049,307.00 | 17,950,693.00 | 100 |
| 5 | MIRADI MIKAKATI - STENDI | 600,000,000.00 | 600,000,000.00 | - | 600,000,000.00 | 538,660,235.00 | 61,339,765.00 | 100 |
| 6 | UJENZI WA ZAHANATI YA NYERERE | 50,000,000.00 | - | - | - | | - | - |
| 7 | UJENZI WA ZAHANATI YA NIUMBA | 50,000,000.00 | - | - | - | | - | - |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | MPANGO WA KUINUA ELIMU (SEQUIP) | 5,209,900,000.00 | 3,000,000,000.00 | - | 3,000,000,000.00 | 982,113,923.00 | 2,017,886,077.00 | 58 |
| 9 | MIRADI YA KUPAMBANA NA MALARIA,TB,HIV | 29,159,000.00 | 7,364,624.30 | - | 7,364,624.30 | 7,364,624.30 | - | 25 |
| 10 | MRADI WA KUPAMBANA NA MAGONJWA YASIYOPEWA KIPAOMBELE - NTD | 15,549,000.00 | - | - | - | | - | - |
| 11 | MIRADI YA HUDUMA ZA MAJI, ELIMU YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA - SWASH | 37,000,000.00 | - | - | - | | - | - |
| 12 | MIRADI YA WALTEREED | 204,589,000.00 | 117,195,290.66 | - | 117,195,290.66 | 117,195,290.66 | - | 57 |
| 13 | RUZUKU YA MIRADI - UNICEF | 229,763,000.00 | 116,886,581.00 | - | 116,886,581.00 | 116,150,000.00 | 736,581.00 | 51 |
| 14 | MFUKO WA AFYA WA PAMOJA (BASKET FUND) | 28,342,200.00 | 37,016,076.98 | 75,591,912.00 | 112,607,988.98 | 112,607,988.98 | - | 397 |
| 15 | MIRADI YA TASAF | 407,524,000.00 | 272,292,000.00 | - | 272,292,000.00 | 272,292,000.00 | - | 67 |
| 16 | UVIKO - 19 - CHANJO | | 27,380,848.22 | 9,250,000.00 | 36,630,848.22 | 36,630,848.22 | - | |
| | **JUMLA YA MIRADI NGAZI YA HALMASHAURI** | **8,446,826,200.00** | **5,763,135,421.16** | **84,841,912.00** | **5,847,977,333.16** | **3,703,181,558.54** | **2,144,795,774.62** | **69** |

**MIRADI YA MAENDELEO INAYOTEKELEZWA KATIKA NGAZI ZA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA - RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU NA WAHISANI**

| NA | MAELEZO | MAKISIO YA MWAKA 2021/2022 | MAPOKEZI KUANZIA JULAI-APRILI,2022 | MAPOKEZI KWA MWEZI MEI 2022 | JUMLA YA MAPOKEZI JULAI-MEI,2022 | | TOFAUTI YA MAKISIO NA MAPOKEZI HALISI | (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ELIMU BILA MALIPO - ELIMU MSINGI | 410,058,000.00 | 342,182,914.68 | 36,301,379.00 | 378,484,293.68 | 378,484,293.68 | - | 92 |
| 2 | ELIMU BILA MALIPO ELIMU - SEKONDARI | 427,700,000.00 | 333,355,323.69 | 34,999,578.00 | 368,354,901.69 | 368,354,901.69 | - | 86 |
| 3 | MPANGO WA KUINUA ELIMU (SEQUIP) | 729,500,000.00 | - | - | - | | - | - |
| 4 | MFUKO WA AFYA WA PAMOJA (BASKET FUND) | 160,605,800.00 | - | - | - | | - | - |
| 5 | UKAMILISHAJI WA MADARASA ELIMU MSINGI | 112,500,000.00 | 112,000,000.00 | - | 112,000,000.00 | 112,000,000.00 | - | 100 |
| 6 | UKAMILISHAJI WA MADARASA ELIMU SEKONDARI | 112,500,000.00 | 112,500,000.00 | - | 112,500,000.00 | 112,500,000.00 | - | 100 |
| | UKAMILISHAJI WA MADARASA SEKONDARI | | 37,500,000.00 | | 37,500,000.00 | 37,500,000.00 | - | |
| 7 | UKAMILISHAJI WA VYUMBA VYA MAABARA | 125,000,000.00 | 125,000,000.00 | - | 125,000,000.00 | 125,000,000.00 | - | 100 |
| 8 | FEDHA ZA LIPA KULINGANA NA MATOKEO (EP4R) | 693,163,000.00 | - | - | - | | - | - |
| 9 | UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 | - | 1,000,000,000.00 | 788,621,177.43 | 211,378,822.57 | 100 |
| | COVID-19(MABWENI MSINGI) | | 80,000,000.00 | - | 80,000,000.00 | 80,000,000.00 | - | - |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | COVID-19(MADARASA SEKONDARI) | | 1,040,000,000.00 | - | 1,040,000,000.00 | 1,040,000,000.00 | - | - |
| | COVID - 19(MADARASA SHULE SHIKIZI) | | 40,000,000.00 | - | 40,000,000.00 | 40,000,000.00 | - | - |
| | COVID-19(NYUMBA ZA WATUMISHI) | | 90,000,000.00 | - | 90,000,000.00 | | 90,000,000.00 | |
| | COVID-19(MAJENGO HUDUMA ZA DHARURA | | 300,000,000.00 | - | 300,000,000.00 | 261,712,697.06 | 38,287,302.94 | |
| | COVID-19(UHAMASISHAJI WA CHANJO) | | 20,251,075.51 | - | 20,251,075.51 | | 20,251,075.51 | |
| | COVID-19(UFUATILIAJI NA TATHMINI) - 78J10 | | 6,514,747.00 | - | 6,514,747.00 | | 6,514,747.00 | |
| | UJENZI KITUO CHA AFYA MWAKAKATI | | 500,000,000.00 | - | 500,000,000.00 | 438,564,326.23 | 61,435,673.77 | - |
| | UJENZI KITUO CHA AFYA CHAPWA | | 500,000,000.00 | - | 500,000,000.00 | | 500,000,000.00 | - |
| | UJENZI WA MAENEO YA WAMACHINGA | | 383,000,000.00 | - | 383,000,000.00 | 383,000,000.00 | - | - |
| | FEDHA ZA CHANJO YA POLIO | | 21,320,950.00 | - | 21,320,950.00 | | 21,320,950.00 | |
| 10 | UNUNUZI WA VIFAA TIBA | 500,000,000.00 | 376,600,000.00 | | 376,600,000.00 | 376,600,000.00 | - | 75 |
| 11 | UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA - LANES | 64,000,000.00 | - | - | - | - | - | - |
| | **JUMLA YA MIRADI NGAZI YA VITUO VYA HUDUMA** | **4,335,026,800.00** | **5,420,225,010.88** | **71,300,957.00** | **5,491,525,967.88** | **4,542,337,396.09** | **949,188,571.79** | **126.68** |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **JUMLA KUU YA MIRADI YA MAENDELEO (SERIKALI KUU)** | **12,781,853,000.00** | **10,712,039,482.04** | **156,142,869.00** | **11,339,503,301.04** | **8,245,518,954.63** | **3,093,984,346.41** | **88.72** |
| 12 | MIRADI YA MAENDELEO KWA MAPATO YA NDANI | 4,333,254,300.00 | 4,316,972,267.00 | 4,398,188,982.00 | 354,000,000.00 | 3,678,420.285.00 | -64,934,682.00 | 101.4 |
| | **JUMLA KUU YA MIRADI YA MAENDELEO** | **17,115,107,300.00** | **15,029,011,749.04** | **4,554,331,851.00** | **19,583,343,600.04** | **8,245,518,954.63** | | |

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI, MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KUTOKA DIVISHENI NA VITENGO MBALIMBALI**

- **DIVISHENI YA MAENDELEO YA JAMII**

**Mhe.Mwenyekiti**

Divisheni ya Maendeleo ya Jamii imefanya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kiutendaji kwa kuratibu majukumu ya Divisheni katika Seksheni kwa kuzingatia Malengo ya mwaka **2021/2022** kama ifuatavyo:-

1. Kuhakikisha Jamii inashiriki katika kuanzisha, kutekeleza na kusimamia miradi mbalimbali ya Jamii na shughuli za kujitegemea kwa katumia rasilimali za ndani na nje ya Jamii na utekelezaji wake ni kwamba;

Kufanyika kwa ushawishi na uhamasishaji kwenye mikutano ya jamii ili kuweza kushiriki katika Miradi ya Maendeleo inayoanzishwa na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi iliyopokea Fedha za Halmashauri kutokana na mapato ya ndani kwenye miradi ya Divisheni za Elimu, Afya na Ujenzi

2. Kupunguza maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI kwa lengo la kufikia 90, 90, 90. (90% kupima na kujitambua, **90%** waliotambuliwa kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU/UKIMWI, 90% Kuondoa unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI), Utekelezaji wake ni kwamba:

i. Kufanyika kwa uhuwishaji na mafunzo ya Kamati 6 za kudhibiti UKIMWI katika kata za Katete, Mpemba, Chapwa, Sogea, Makambini na Maporomoko;
ii. Kufanyika kwa maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani tarehe 01/12/2021 katika kata ya Tunduma Mtaa wa Sikanyika;
iii. Kuwezesha ujenzi wa ofisi bora ya KONGA la Watu Wanaoishi na VVU ambapo ujenzi utafanyika kata ya Tunduma Mtaa wa Ihanda na kuunda na kuwezesha mikopo ya 10% vikundi viwili vya WAVIU.

3. Kuwezesha maadhimisho mbalimbali yanayoihusu sekta ya maendeleo ya jamii. Utekelezaji wake ni kwamba;

i. Kumefanyika maadhimisho ya siku ya Wanamke duniani siku ya tarehe 07/03/2022 kata za Uwanjani;

ii. Maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika Kufanyika kwa maadhimisho ya siku ya ya tarehe 14-15/06/2022 kwa kutoa Elimu ya jinsia na kupinga ukatili kwa watoto Kata za Chiwezi Mtaa wa Namole kwa wanafunzi wa sekondari na shule ya msingi

iii. Kumefanya maadhimisho ya siku ya Wajane Duniani ambapo yalipelekea kupata vikundi

4. Uwezeshaji wananchi kiuchumi na kupunguza umaskini utekelezaji wake ni kwamba;

i. Utoaji wa mikopo 10% kwa vikundi umefanyika kwa vikundi 39 vya wanawake vyenye wanufaika 332 (Tsh 281,283,620), vijana vikundi 36 vyenye wanufaika 133(Tsh 318,483,810) na kiasi cha (Tsh 120,841,810) zimekopeshwa kwa watu 18 wenye ulemavu.

ii. Kufanyika kwa ufuatiliaji wa marejesho na maendeleo ya miradi ya vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu vilivyonufaika na mikopo ambapo fedha za marejesho kiasi cha Tsh 764,100,000 zilifanikisha kukopesha vikundi vya wanawake 10 kwa TSh 177,000,000.00 na vikundi vya vijana 21 kwa Tsh 587,100,000/= kati ya hizo jumla ya pikipiki 229 kwaajili ya vikundi vya Bodaboda

iii. Umefanyika uratibu wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambapo Halmashauri imewezesha uhawilishaji fedha kwa walengwa wa Kaya masikini 1,677 katika mitaa 68 ambapo jumla ya malipo ya kiasi cha 355,884,000/= yalifanyika

5. Kuhakikisha masuala ya jinsia na watoto yanaratibiwa na kuingizwa katika utekelezaji wa mipango na afua mbalimbali ambapo utekelezaji wake ni kwamba;

i. Kufanyika kwa ufuatiliaji na usimamizi wa utendaji kazi wa kamati za MTAKUWWA na utoaji elimu kuhusu uimalishaji wa kamati umefanyika katika kata ya zote

ii. Kufanyika kwa mikutano ngazi ya jamii kwa kutoa ‘Key Message’ ili kuelimisha jamii madhara ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto katika jamii kwa kushirikiana na kikundi cha KIWAWASO

**Changamoto zilizojitokeza**

i. Kutokidhi vigezo kutokana na miradi iliyoombewa mkopo kutoonyeha uhalisia wa umiliki wa mradi

ii. Baadhi ya vikundi vimeombea shughuli za ununuzi wa mazao na samaki kuwa na wanachama ambao hawajihusishi na shughuli hiyo moja kwa moja na kutoonesha umiliki wa mradi kama kikundi.

iii. **Utatuzi wa changamoto zilizojitokeza**

1. Kufanya mikutano ngazi ya Kata kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii juu ya uundaji wa vikundi kulingana na aina ya mradi pamoja na kuwaelimisha taratibu za uombaji mkopo na taratibu za marejesho kwa mujibu wa sharia ma kanuni
2. Kuhamasisha vikundi vya walemavu na wenye ulemavu – binafsi ili kuitambua fursa hiyo ya mikopo ikiwa ni pamoja
3. Kuelimisha vikundi vya vijana suala la kuzingatia umri katika maombi ya mikopo

**Mipango ya baadaye**

1. Kuendelea Kuamsha Ari ya Jamii kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo
2. Kuendelea kuunda mabaraza ya watoto kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na Watoto
3. Kutoa elimu ngazi ya Jamii kuhusu taratibu za unufaikaji wa mikopo ya 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wanavikundi kuhakikisha wanajiandikisha kupata Namba za NIDA ambalo ni takwa muhimu kwa vikundi vyote vitakavyokuwa vinaomba mkopo kwa mwaka huu wa fedha **2022/2023** na kuendelea.
4. Kufanya ufuatiliaji mwenendo wa marejesho ya mkopo iwe endelevu ikiwa ni pamoja na kukagua maendeleo ya miradi ya vikundi kwakuwa usafiri kwa sasa sio tatizo baada ya kupatikana magari mapya
5. Kitengo cha Huduma za Sheria kuendelea kukazia hukumu za vikundi 39 na kufungua mashtaka kwa vikundi vingine **21** ambavyo vipo nje ya muda wa kufanya marejesho.

- **DIVISHENI YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

**Mhe.Mwenyekiti**

Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Divisheni ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inajumuisha takwimu za viwanda vidogo,ushuru wa malazi, ushuru wa huduma na utoaji leseni za biashara.

- **Hali ya Viwanda katika Mji wa Tunduma**

Halmashauri ya Mji Tunduma ina jumla ya viwanda vidogovidogo **531,** ikiwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeweza kusajili jumla ya mashine za kusaga na kukoboa 11na mashine 1 ya mpunga.

- **Leseni za Biashara**

**Mhe.Mwenyekiti**

Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** ilikisiwa kukusanya jumla ya Tshs.**320,000,000.00** ikiwa ni ada za Leseni lakini hadi kufikia Juni **30**, **2022** Jumla ya Tshs. **394,910,478.92** zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia **123.41**

| **Makisio kwa mwaka 2021/2022** | **Makusanyo halisi kwa mwaka 2021/2022** | **Asilimia ya makusanyo yote kwa mwaka** |
|---|---|---|
| 320,000,000.00 | 394,910,478.92 | 123.41 |

**1.2 Leseni za Vileo**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikisiwa kukusanya Jumla ya Tshs.**12,600,000.00** kutoka kwenye Leseni za vileo lakini hadi kufikia Juni, 30,2022 jumla ya Tshs **22,943,000.22** zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia **182.09**

| **Makisio kwa mwaka 2021/2022** | **Makusanyo halisi kwa mwaka 2021/2022** | **Asilimia ya makusanyo yote kwa mwaka** |
|---|---|---|
| **12,600,000.00** | **22,943,000.22** | **182.09** |

- **Ushuru wa malazi**

**Mhe.Mwenyekiti**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikisiwa kukusanya Jumla ya Tshs.**120.000,000.00** kutoka kwenye Ushuru wa Malazi, lakini hadi kufikia Juni, **30, 2022** jumla ya Tshs **211,853,770.00** zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 176.54.

| **Makisio kwa mwaka 2021/2022** | **Makusanyo halisi kwa mwaka 2021/2022** | **Asilimia ya makusanyo yote kwa mwaka** |
|---|---|---|
| **120,000,000.00** | **211,853,770.00** | **176.54** |

- **Ushuru wa Huduma (Service Levy)**

**Mhe.Mwenyekiti**

Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** imekisiwa kukusanya jumla ya Tshs.**242.000,000.00** kutoka kwenye Ushuru wa Huduma lakini hadi kufikia Juni, 30,2022 jumla ya Tshs **511,235,977.77** zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia **211.25.**

| Makisio kwa mwaka 2021/2022 | Makusanyo halisi kwa mwaka 2021/2022 | Asilimia ya makusanyo yote kwa mwaka |
|---|---|---|
| **242,000,000.00** | **511,235,977.77** | **211.25** |

- **DIVISHENI YA MIUNDOMINU MAENDELEO YA VIJIJINI NA MIJINI**

**Mhe.Mwenyekiti**

Katika kipindi cha mwaka **2021/2022,** Divisheni ya Miundombinu Maendeleo ya Vijijini na Mijini imefanya kazi zake za kusimamia miradi mbalimbali pamoja na kusimamia zoezi za utoaji vibali vya ujenzi kwa kushirikiana na Seksheni ya Ardhi na Mipangomiji kama ilivyochanganuliwa katika majedwali.

**JEDWALI LA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA DIVISHENI YA MIUNDOMBINU MAENDELEO YA VIJIJINI NA MIJINI KWA MWAKA 2021/2022**

| NA | LENGO LA MWAKA | LENGO LA MWAKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | Kusimamia miradi ya ujenzi kuwa katika ubora na kwa kuzingatia thamani ya pesa (value for money). | Kufanya usimamizi wa miradi ya ujenzi ifuatayo:<br><br>1.Ujenzi wa shule ya sekondari Tunduma TC iliyopo maporomoko.<br>2.Madarasa na vyoo kwa shule za Msingi.<br>3.Ukarabati wa ofisi ya Mbunge kata ya Tunduma.<br>4.Madarasa na vyoo kwa shule za Sekondari.<br>5.Ujenzi wa stendi ya mabasi.<br>6.Ukarabati wa soko la mazao<br>7.Ujenzi wa Hospitali ya Mji Tunduma<br>8.Ujenzi wa kituo cha afya Chapwa<br>9.Ujenzi wa kituo cha afya Chiwezi<br>10.Ujenzi wa kituo cha afya Chipaka<br>11.Ujenzi wa madarasa 54 kwa fedha za UVIKO 19.<br><br>12.Ujenzi wa kituo cha Afya Mwakakati | 1.Ujenzi wa shule ya sekondari Tunduma TC iliyopo maporomoko umetekelezwa **90%**<br>2. Ujenzi wa Hospitali ya Mji Tunduma awamu ya sita imetekelezwa 85%<br>3.Madarasa na vyoo kwa shule za Msingi umetekelezwa kwa 100%.<br>4.Ukarabati wa ofisi ya Mbunge kata ya Tunduma umetekezwa kwa 99%.<br>5.Madarasa na vyoo kwa shule za sekondari umetekelezwa kwa 100%.<br>6.Ujenzi wa stendi ya mabasi umetekeleza kwa 75%.<br>7.Ujenzi wa kituo cha afya Chapwa umetekelezwa kwa **87%.**<br><br>8.Ukarabati wa soko la |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 13.Ujenzi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji Tunduma<br>14.Ujenzi wa Jengo la Dharura EMD<br>15.Ujenzi wa nyumba ya mkurugenzi<br>16.Ujenzi wa Shule Uwanjani<br>17.ujenzi wa nyumba ya mtumishi 3 in 1 chiwezi<br>18.Ujenzi wa Uwanja wa mpira chapwa<br>19.Ujenzi wa shule ya msingi Haisoja<br>20.Ujenzi Restaurant na Rest House<br>21.Ujenzi wa Kituo cha Afya Mpande<br>22. Ujenzi wa soko la machinga Majengo<br>23.Ujenzi wa shule ya wasichana Namole | mazao umetekelez100%<br>9.Ujenzi wa kituo cha afya Chiwezi umetekelezwa kwa 92%<br>10.Ujenzi wa kituo cha afya Chipaka 98 %<br>11.Ujenzi wa madarasa 54 kwa fedha za UVIKO 19 umekamilika kwa 100%<br>12.Ujenzi wa kituo cha Afya Mwakakati umekamilika kwa 63%<br>13.Ujenzi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji Tunduma awamu ya II umekamilika kwa 89%<br>14.Ujenzi wa Jengo la Dharura EMD umekamilika kwa 89%<br>15.Ujenzi wa nyumba ya mkurugenzi umekamilika kwa 80%<br>16.Ujenzi wa Shule Uwanjani umekamilika kwa 65%<br>17.ujenzi wa nyumba ya mtumishi 3 in 1 chiwezi umekamilika kwa 85%<br>18.Ujenzi wa Uwanja wa mpira chapwa umekamilika kwa 25%<br>19.Ujenzi wa shule ya Msingi Haisoja umekamilika kwa 65%<br>20. Ujenzi Restaurant na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Rest House umekamilika kwa 56%<br>21. Ujenzi wa Kituo cha Afya Mpande Umekamilika kwa 13%<br>22. Ujenzi wa soko la machinga Majengo umekamilika kwa 10%<br>23. Ujenzi wa shule ya wasichana Namole umekamilika kwa<br>**18%** |
| 2 | Kusimamia na kutoa vibali vya ujenzi wa Majengo ya Taasisi na watu binafsi katika Halmashauri ya Mji Tunduma | Kupitisha ramani na kutoa vibali vya Ujenzi. | Jumla ya Ramani na vibali vilivyotolewa kwenye robo ya pili ni.<br>• Makazi- 219<br>• Biashara- 17<br>• Makazi/Biashara-8<br>• Taasisi-10<br>• Fence-14<br>• Frames-1<br>• Godown-1<br>• Filling station-2<br>• Guest House-1 |
| 3 | Kuandaa taarifa mbalimbali za kila wiki na taarifa za utekelezaji wa miradi kila robo. | Kuandaa taarifa za kila wiki na taarifa moja za robo ya tatu | Taarifa za wiki na moja ya robo ya Nne imeandaliwa na kuwasilishwa kikamilifu ambayo ni sawa na 100% ya utekelezaji wa lengo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4<br>` | Kuainisha barabara za kufungua kwa lengo la kuzitambua na hatimaye kuzifungua. | Kuainisha barabara zote za kuelekea kwenye maziko zilizopo kwenye mpango na kuhamisha fedha za barabara kwenda Tarura kwa ajili ya kufungua | Jumla ya fedha kiasi cha Tshs.**135,000,000** tayari zimeshapelekwa mchanganuo wa barabara za kuzifungua zimesha ainishwa ambazo ni barabara ya Chapwa A -Mpakani-Makaburini km 1.23, Mpemba stendi- makaburini km1 na Ipito Makaburini km 0.38 |
| 5 | Kuandaa makisio ya miradi ya ujenzi wakati wa kuandaa miradi. | Kuandaa makisio na kupata gharama za awali za mradi. | Jumla ya miradi **114** imeandaliwa makisio kwa mwaka **2021/2022** |

- **DIVISHENI YA ELIMU MSINGI NA ELIMU YA AWALI 2021/2022.**

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji wa Tunduma ina jumla ya shule za Msingi za Serikali **49** zenye jumla ya Wanafunzi **46,648** kuanzia darasa la Awali hadi la saba (Wavulana **23273**; Wasichana **23375**). Kuna wanafunzi **4,112** wa Elimu ya Awali, ikiwa wavulana ni **2041** na wasichana **2,071.** Shule za msingi za binafsi ziko 14 zenye jumla ya wanafunzi **2,728** pamoja na Awali ikiwa Wavulana ni **1,368** na Wasichana **1,360** Shule za msingi za Binafsi zina jumla ya Wanafunzi **460** wa Awali, ikiwa Wavulana ni **206** na Wasichana **254.** Hivyo Halmashauri ya Mji Tunduma ina jumla ya wanafunzi **49,376** kuanzia Darasa la Awali hadi Darasa la VII.

**Taarifa ya matokeo ya mtihani wa Taifa Darasa la Nne na Darasa la Saba 2021**

| DARASA | WALIOFANYA | | | WALIOFAULU | | | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | |
| VII | 1998 | 2121 | 4119 | 1820 | 1923 | 3743 | 91 |
| IV | 2457 | 2640 | 5097 | 2309 | 2535 | 4844 | 95 |

**Taarifa ya uandikishaji awali na Darasa la kwanza 2022**

| DARASA | MAOTEO | WALIOANDIKISHWA | % |
|---|---|---|---|
| AWALI | 4145 | 4572 | 110 |
| I | 5790 | 7480 | 129 |

- **DIVISHENI YA ELIMU SEKONDARI**

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji Tunduma ina jumla ya shule za Sekondari **19**, kati ya shule hizo shule **14** zinamilikiwa na serikali na shule **05** ni za watu binafsi, kati ya shule **14** za Serikali shule zenye Kidato cha Kwanza hadi cha Sita ni **03**, Shule hizo zina jumla ya wanafunzi **10244** (Wav **4735**, Was **5509**), wanafunzi wa shule za Serikali ni **9320**, ikiwa (Wav **4339**, Was **4981**) na wanafunzi wa shule binafsi ni **924**, ikiwa (Wav **396**, Was **528**).

**1.0 MAHITAJI YA WALIMU**

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji Tunduma ina upungufu wa Walimu hasa wa masomo ya sayansi kulingana na ongezeko la idadi ya wanafunzi kama inavyoonesha kwenye jedwali hapa chini;

| **SAYANSI** | | | **SANAA** | | | **MAHITAJI YA JUMLA** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mahitaji** | **Waliopo** | **Upungufu** | **Mahitaji** | **Waliopo** | **Upungufu** | **Mah** | **Waliopo** | **Upungufu** |
| 161 | 83 | 78 | 194 | 184 | 10 | 355 | 267 | 88 |

**Mapokezi ya wanafunzi Kidato cha Tano mwaka 2022**

| **NA** | **SHULE** | **WALIOPANGWA** | | | **Walioripoti** | **Wasioripoti** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Awamu I | Awamu II | JUMLA | | |
| 1 | Mwl.J.K.Nyerere | 122 | 5 | 127 | 96 | 31 |
| 2 | Mpemba | 162 | 14 | 176 | 96 | 80 |
| 3 | Tunduma TC | 130 | 6 | 136 | 80 | 56 |
| | **Jumla** | **414** | **25** | **439** | **272** | **167** |

**Mapokezi ya Walimu ajira mpya mwaka 2022**

Divisheni ya Elimu Sekondari, imepangiwa jumla ya walimu **33** (Me 27, Ke 6) Walimu hao wanatakiwa kuanza kuripoti Julai 2022 kulingana na vituo/ shule walizopangiwa.

**Matokeo ya Kidato cha Sita Mwaka 2021/2022**

Wanafunzi waliosajiliwa na kufanya mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2022, walikuwa 162 ( wav 100, was 62) na matokeo yao ni kama yanavyoonesha hapa chini

| NA | SHULE | WALI OFAN YA | DIVISI ON I | DIVISI ON II | DIVISIO N III | DIVISIO N IV | % | NAFASI - MKOA | NAFASI KITAIFA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MWL.J.K.NYE RERE | 100 | 30 | 57 | 13 | 0 | 100 | 4 KATI YA 11 | 265 KATI YA 644 |
| 2 | MPEMBA | 62 | 14 | 44 | 4 | 0 | 100 | 6 KATI YA 11 | 305 KATI YA 644 |
| | **JUMLA** | **162** | **44** | **101** | **17** | **0** | | | |

**Changamoto zilizojitokeza na namna ya kuzitatua**

Kuna changamoto zilizojitokeza ni kama ifuatavyo;

- Pamoja na kupangiwa walimu, upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi

  **Utatuzi wake**- Shule zinatumia walimu wa muda ili kupunguza tatizo la upungufu wa walimu

**DIVISHENI YA UTAWALA NA RASLIMALI WATU**

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji Tunduma ilianzishwa tarehe **01** Julai **2015** ikiwa na Muundo wa Kiutawala wa **Tarafa Moja (01)** ya Tunduma, **Kata 15** na **Mitaa 71**. Muundo wa Kimajukumu Halmashauri imegawanyika katika Idara **13** na Vitengo **6**.Halmashauri ya Mji Tunduma ina jumla ya watumishi 1075 mahitaji ya watumishi ni 1325 upungufu ni watumishi 250 kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo chini.

- **Mishahara ya Watumishi**

**Mhe. Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji Tunduma imeweza kutenga na kulipa mishahara ya watumishi kwa muda wa miaka mitatu kama ifuatavyo.

Kwa mwaka wa fedha **2020/2021** Halmashauri ya Mji wa Tunduma ilitenga na iliidhinishiwa kiasi cha **Tshs 15,492,069,000** ikiwa ni kwaajili ya mishahara, ajira mpya, upandaishaji wa vyeo,nyongeza za mishahara na kubadilisha miundo ya utumishi.

Hivyo kwa mwaka wa fedha **2020/2021**Halmashauri ililipa Mishahara kwa Watumishi **1027** ambao walitumia jumla ya **Tshs 9,172,360,600.00.** Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Mji Tunduma ilitenga na kuidhinishiwa kiasi cha **Tshs**.**12,434,717,348.00** kwa ajili ya malipo ya mishahara, nyongeza za mishahara,upandaji wa vyeo,kubadilisha miundo ya utumishi na ajira mpya.

- **Utekelezaji wa malipo ya stahiki mbalimbali za watumishi**

**Mhe.Mwenyekiti**

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Halmashauri iliidhinishiwa jumla ya watumishi **467** kupanda vyeo na imefanikiwa kupandisha vyeo jumla ya watumishi 351 katika Idara zote pia Halmashauri ya Mji Tunduma iliidhinishiwa kubadilisha miundo watumishi 18 lakini imefanikiwa kubadilisha miundo watumishi **46.**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilitenga kiasi cha Tshs **116,423,825** kwa ajili ya upandishaji wa vyeo kwa watumishi **90,** hata hivyo upandishwaji vyeo haukufanyika kutokana na Ikama (Mwongozo) ya upandishwaji vyeo kutotolewa, Aidha serikali imetoa maelekezo ya ubadilishaji wa miundo kwa watumishi waliojiendeleza ambao mabadiliko yao hayaathiri bajeti ya Mishahara ambapo jumla ya watumishi 27 wamebadilishiwa miundo ya utumishi mpaka Juni **2021**.

**Likizo**

Halmashauri ya Mji Tunduma katika kushughulikia stahiki mbalimbali za watumishi imekuwa ikiwapa likizo watumishi kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Utumishi wa umma za mwaka 2009 na kuhakikisha wanalipwa stahiki zao za likizo kama ifuatavyo;

Kwa mwaka wa fedha **2020/2021** jumla ya watumishi **479** waliokuwa na likizo za malipo waliruhusiwa kwenda likizo na kulipwa kiasi cha **Tshs 64,985,000/=**

Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Mji Tunduma imefanikiwa kulipa jumla ya **Tshs 80,791,800.00** mpaka Juni **2022** kwa ajili ya likizo na kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Halmashauri imetenga kiasi cha **Tshs 150,000,000** kwa ajili ya malipo ya likizo.

- **Malipo ya fedha ya kujikimu kwa ajira mpya.**

**Mhe.Mwenyekiti**

Kwa kuzingatia umuhimu wa watumishi ajira mpya Halmashauri imekuwa ikitenga bajeti ya fedha ya kujikimu kwa watumishi ajira mpya.

Kwa mwaka wa fedha **2020/2021** Halmashauri imelipa kiasi cha **Tshs 15,201,000** na kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri imelipa kiasi cha **Tshs 25,480,500** kwa ajili ya kujikimu watumishi ajira mpya.

- **Madeni ya watumishi**

**Mhe.Mwenyekiti**

Kwa mwaka wa fedha **2019/2020**, **2020/2021** na **2021/2022** Halmashauri ilifanikiwa kuwasilisha madai ya watumishi **598** Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora yenye thamani ya Tshs **1,293,237,562**. Watumishi waliolipwa ni **475** jumla ya Tshs **673,186,438** sawa na asilimia **52.1.%**.

**Mhe.Mwenyekiti**

Penye mafanikio hapakosi changamoto, Halmashauri ya Mji Tunduma ina changamoto mbalimbali kama ifuatavyo;-

- **Upungufu wa Watumishi.**

Kwa mujibu wa ikama Halmashauri inatakiwa kuwa na watumishi jumla **1325** mpaka sasa kuna watumishi **1075** upungufu mkubwa wa watumishi **250** upo katika Idara ya Utawala hasa Madereva, Watunza kumbukumbu na Makatibu Muhtasi,Divisheni ya Afya,Ustawi wa Jamii na Huduma za Lishe kutokana na kuongezeka kwa Hospitali ya Mji 1,Vituo vya Afya vitatu, na Zahanati **3,** Divisheni ya ya Elimu Sekondari hasa walimu wa masomo ya Sayansi, Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi hasa katika shule mpya zilizojengwa na kusajiliwa kwa mwaka 2020/2021 na Divisheni ya Kilimo,Mifugo na Uvuvi.

- **Ukomo mdogo wa bajeti ya Mishahara kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

Kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Halmashauri ya Mji Tunduma imepokea ukomo wa bajeti ya mishara ikiwa ni pamoja na makisio ya ajira mpya, upandishaji wa vyeo ubadilishaji wa miundo na nyongeza za mishahara yenye jumla ya Tshs. **10,702,764,542.38** wakati mahitaji ya bajeti ya mishahara kwa watumishi waliopo kazini (Existing Employee Amount ni Shs.**10,352,640,000.00**) Hivyo utekelezaji wa uingizaji wa bajeti kwenye mfumo kuwa mgumu na kupelekea watumishi kukosa bajeti kwaajili ya upandishaji wa vyeo,ajira mpya na ubadilishaji wa miundo ya utumishi.

Kutokana na changamoto hii tunaomba kuongezewa ukomo wa bajeti ya Mishahara ili tukamilishe uingizaji wa bajeti katika mfumo wa mishahara.

- **SEKSHENI YA MAENDELEO YA MJI (ARDHI NA MIPANGOMIJI)**



Seksheni ya maendeleo ya Mji Halmashauri ya Mji wa Tunduma ina Vitengo vinne (4) ambavyo vinafanya kazi kwa kutegemeana katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, na vitengo hivyo ni kama ifuatavyo: -

a) MipangoMiji
b) Upimaji na Ramani
c) Usimamizi wa Ardhi
d) Uthamini

Shughuli kuu zinazofanywa na Seksheni kila siku kwa maendeleo ya Mji ili kukidhi mahitaji ya wananchi ni kama ifuatavyo;

- Usimamizi wa miliki Ardhi na matumizi ya ardhi.
- Utayarishaji mipango ya kina (Detailed Plans) na usimamizi wa maendeleo ya Mji (development control).
- Upimaji wa Ardhi na uandaaji wa ramani za upimaji.
- Uthamini wa mali za umma na watu binafsi kwania ya kulipa fidia, kuuza, kubadili miliki na kukadiria tozo mbalimbali za Serikali.

**Changamoto**

1. Ucheleweshaji wa kuidhinisha michoro ya mipangomiji na ramani za upimaji
2. Upungufu wa wataalamu wa kutosha hasa wapimaji.
3. Ukosefu wa gari kwa ajili ya shughuli za Ardhi.
4. Ufinyu wa bajeti ya Idara ya Mipangomiji.

**Malengo ya Seksheni kwa mwaka 2022/2023**

- Kusambaza ilani za wadaiwa wote wa kodi ya pango la Ardhi ili kufikia malengo ya ukusanyaji tulio pangiwa.
- Kuelimisha, Kufuatilia na Kutoa vibali vya ujenzi ili kuepuka uendelezaji wa mji usiofuata mipango (ujenzi holela)
- Kuendelea na taratibu wa kusimamia utelekezaji wa Mpango Kabambe (Master Plan) ya mji wa Tunduma.
- Kuelimisha na kushawishi wananchi wafuate mpango wa sasa wa upimaji bila fidia ili kuepuka migogoro iliyokuwepo na kuzuia migogoro mipya ya fidia kuibuka.
- Kuendelea kukusanya maduhuri ya Serikali kuu kutoka vyanzo vyote vinavyo husisha Idara ya Mipangomiji.
- Kutoa hati miliki kwa viwanja vilivyopimwa.
- Kutatua migogoro ya Ardhi.

- **DIVISHENI YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**

**Mhe.Mwenyekiti**

Kwa Mwaka wa fedha **2021/2022,** Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama kuandaa mashamba darasa 45 katika kata Sita za uzalishaji, Kuboresha Huduma za Ugani kwa kununua Pikipiki 3 za Maafisa Ugani, kukarabati Soko la Mazao Majengo kwa Kumimina zege kwenye barabara yenye urefu wa mita 250 na Upana wa Mita **7**, Upimaji wa Afya ya udongo kwa Wakulima, ikarabati wa machinjio ya Sogea na Mpemba, Kutoa Chanjo ya Kimeta kwa ng'ombe, Mbuzi na Kondoo, Kutoa mafunzo Kwa Vikundi **5** vya Wafugaji wa ng'ombe na Kuku vilivyopata Mikopo ya 10%, kufanya ukaguzi wa maduka ya Pembejeo za Kilimo na Mifugo, kufanya ukaguzi wa mabucha na usimamizi wa mapato yatokanayo na vyanzo vya Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa ujumla shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha **2021/2022** ni kama zifuatazo;

| NA. | SHUGHULI ILIYOPANGWA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Kuandaa Mashamba Darasa 46 katika kata Sita Za Uzalishaji, | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |
| 2 | Kuboresha huduma za Ugani kwa kununua Pikipiki 3 za Maafisa Ugani | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |
| 3 | Kukarabati Soko la Mazao Majengo kwa Kumimina zege Kwenye Barabara yenye urefu wa Mita 250 na upana wa Mita 7 | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |
| 4 | Upimaji wa afya ya udongo kwa Wakulima 44 | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |
| 5 | Ukarabati wa Machinjio ya Sogea na Mpemba, Kutoa Chanjo ya Kimeta Kwa ng'ombe, Mbuzi na Kondoo | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |
| 6 | Kutoa Mafunzo kwa vikundi 5 vya Wafugaji wa ng'ombe na Kuku vilivyopata Mikopo ya 10% Kutoka Halmashauri. | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |
| 7 | Kufanya ukaguzi wa maduka ya Pembejeo za Kilimo na Mifugo | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |
| 8 | Kufanya Ukaguzi wa Mabucha na Usimamizi wa Mapato yatokanayo na Vyanzo vya Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi | Utekelezaji umefanyika kwa 100% |

- **KITENGO CHA HUDUMA ZA KISHERIA**

**TAARIFA ZA KESI ZA HALMASHAURI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

i. Halmashauri ya Mji Tunduma inakabiliwa na kesi zifuatazo,

| | | | **AINA YA KESI NA IDADI YAKE.** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Jina la Taasisi** | **Idadi ya Kesi zote** | **Madai** | **Jinai** | **Ardhi** |
| 1 | Halmashauri ya Mji Tunduma | 45 | 42 | - | 3 |

ii. Halmashauri ya Mji Tunduma inakabiliwa na kesi 3 (tatu) zinazotokana na migogoro ya ya Ardhi yenye thamani ya **Tshs.3,100,000,000/=**

iii. Halmashauri ya Mji Tunduma imefunguwa shauri moja la uvamizi wa Ardhi ya Halmashauri eneo lenye thamani ya **Tshs. 46, 400,000/=**

iv. Halmashauri ya Mji Tunduma inakabiliwa na kesi 1 (moja) inazotokana na mgogoro wa wakala eenye thamani ya ya **Tshs. 77,610,186**/=

v. Halmashauri ya Mji Tunduma imefungua mashauri ya madai **42** (Arobaini na mbili) zinazotokana na madeni ya mikopo ya vikundi yenye thamani ya Tshs. **254,404,439**/= ambapo kesi 41 zimetolewa maamuzi na Halmashauri kushinda kesi zote baadhi ya vikundi vinaedelea kulipa madeni yao, sasa tupo katika hatua ya ukaziaji wa Hukumu.

- **KITENGO CHA UDHIBITI WA TAKA NGUMU**

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji unduma ni miongoni mwa Halmashauri tano (5) zinazounda Mkoa wa Songwe. Halmashauri hii ilianzishwa mwaka 2015. Kiutawala Halmashauri ina jumla ya Tarafa 1 ambayo ni Tunduma. Kuna Kata 15, Mitaa 71. kwa upande wa kusini, imepakana na wilaya ya Ileje, Kaskazini imekapakana na Halmashauri ya Momba, mashariki imepakana na wilaya ya Ileje na kwa upande wa magharibi imepakana na Wilaya ya Nakonde (Zambia). Halmashauri ina eneo la kilometa za mraba 419 (sawa 1.6% ya eneo la mkoa wa Songwe). Mji wa Tunduma unakadiriwa kuwa na idadi ya watu 170,026, ni kati ya miji inayokuwa kwa kasi sana nchini kutokana na mwingiliano mkubwa uliopo kutokana na kuwepo kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Inakadiriwa kuzalisha jumla ya tani 400 za taka ngumu kwa siku. Kiwango hicho cha uzalishaji kinajumuisha taka za majumbani, taasisi, sehemu za biashara, masoko na taka kutoka sekta isiyo rasmi.

Halmashauri ya Mji-Tunduma kupitia Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu katika kuhakikisha Usimamizi, uhifadhi/utunzaji na usafishaji wa Mazingira ya mji unaimarishwa na kufanywa kuwa mojawapo ya eneo nyeti linalotiliwa mkazo na serikali katika ngazi zote za kiutawala kwa kuzingatia kuwa sifa na heshima ya mji wowote duniani inaanza kwenye masuala ya usafi (unadhifu wa Mji), kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuepusha magonjwa ya mlipuko na magonjwa ya kuambukiza kama vile kipindupindu na magonjwa ya kuhara.

- **Usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu**

Halmashauri ya Mji Tunduma ni kati ya miji inayokuwa kwa kasi na kibiashara inayopelekea uwepo wa shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazopelekea uzalishaji mkubwa wa taka ngumu kutoka katika maeneo mbalimbali ya biashara, masoko, majumbani unaokadiriwa kufikia takribani tani 136 kwa siku kutoka katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji. Kiasi cha taka kilichoweza kuzalishwa kwa mwaka 2021/2022 inakadiriwa kufikia tani 49,776 ambapo tani 42,956.69 sawa na 86.3% ya taka zote zilizozalishwa kwa mwaka zilipelekwa dampo. Halmashauri ya mji Tunduma imeshika nafasi ya pili (2) kitaifa katika mashindano ya usafi wa mazingira kitaifa katika kundi la halmashauri za mji Tanzania. Hata hivyo halmashauri imeendelea kusimamia suala la usafi wa mazingira kwa kusimamia usafi wa mazingira kwa kila jumamosi ya kila wiki ya mwisho wa mwezi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira ikiwemo wananchi,viongozi wa kisiasa na kidini na wadau wengineo.

Aidha katika kutekeleza masuala yahusuyo usafishaji wa mji ulijumuisha mbinu mbalimbali kama ifuatavyo;

**i. Ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa usafi wa Mazingira ya mji**

Halmashauri kupitia utekelezaji mfumo shirikishi jamii katika usimamizi wa usafi wa Mazingira Mji-Tunduma, Halmashauri ya Mji Tunduma inatoa huduma ya usafi wa mazingira hususani uondoshaji wa taka ngumu kwa namna mbili (2) kwa maana ya ngazi ya Halmashauri na ngazi ya kata, idara imeendelea kuratibu na kusimamia katika kuhakikisha taka zinazozalishwa zinaondoshwa nakupelekwa sehemu ya uteketezaji (Disposal point/Dumpsite) kama sheria ya serikali za mitaa (mamlaka za miji) namba 8 ya mwaka 1982 kifungu cha 53 na 80, sheria ya fedha ya serikali za mitaa namba 9 kifungu cha 13 ya mwaka 1982 na sheria ya usimamizi wa Mazingira namba 20 yamwaka 2004 kifungu cha 38(i) ambayo inazipa mamlaka za miji uwezo huo.

**ii. Kusimamia Usafishaji wa mji na Ukusanyaji wa Taka Ngumu kutoka kwenye majengo, maeneo yawazi, barabara na Mifereji ya kuondoa maji ya Mvua.**

Idara imeendelea kusimamia na kuimarisha usafishaji wa mji ambapo imeajiri vibarua/watumishi wa mkataba 85 wanaofanya shughuli za usafishaji katika maeneo mbalimbali ya mji ikiwemo masoko, barabara kuu, mifereji ya maji ya mvua, stendi, vituo vya kukusanyia taka kwa muda na vyoo. Aidha Idara imeendelea kutumia magari 3 ya kuzolea taka na kuhakikisha mji unakuwa katika hali ya usafi.

iii. **Kusimamia Ukusanyaji wa ada/tozo zitokanazo na huduma ya uzoaji wa taka kila mwezi**

Utekelezaji wa mfumo shirikishi jamii wa utoaji wa huduma za usafishaji na uzoaji wa taka umeendelea kuimarika zaidi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo za usafi na huduma ya uzoaji wa taka ngazi ya kaya (**1000/=**Tsh), na maeneo ya biashara kuanzia **5,000/=** kama sheria ndogo ya usafi wa mazingira ya mji ya mwaka **2017** inavyoelekeza kwa mwezi ambapo mfumo huu umeanzia ngazi ya kata ambapo **80%** ya mapato yanayokusanywa na kata husika yanarudi katani kwa ajili ya huduma ya uzoaji wa taka na 20% inabaki Halmashauri. Mfumo huu umeimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo/ada za usafi ambapo ilipangwa kukusanywa **217,550,000/=**Tsh na kiasi kilichokusanywa kwa mwaka ni **241,140,210/=** Tsh sawa na **111%** ya kiasi kilichopangwa kukusanywa.

iv. **Kusimamia utekelezaji wa mradi wa eneo la kutupia taka (Dumpsite)-Namole**

Halmashauri katika kuhakikisha taka ngumu zote zinazozalishwa zinatupwa katika eneo salama kwa kulinda afya za jamii na mazingira. Mradi unaendelea kutekelezwa kadri ya upatikanaji wa fedha, mpaka sasa ujenzi umefikia asilimia 74. Hata hivyo Tathimini ya athari kwa Mazingira(TAM-Environmental impact assessment-EIA), mchakato wa EIA umefanyika na cheti kimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**v. Utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa Mazingira-Ujenzi wa vyoo bora**

Halmashauri imeendelea kutekeleza kampeni ya ujenzi wa vyoo bora kuanzia ngazi ya kaya, taasisi za kutolea huduma na taasisi zingine, katika utekelezaji wa kampeni hii yafuatayo yamefanyika**.**

- Ufuatiliaji na elimu zimetolewa kupitia Mikutano, Washa/semina na kamati za usafi wa Mazingira ngazi ya jamii (CLTS) mbalimbali ziliundwa kwenye mitaa (38) na kata saba (7) kuhakikisha kila kaya, taasisi zinakuwa na vyoo bora.
- Uwezeshaji wa kamati za usafi wa Mazingira ngazi ya jamii (CLTS) kwenye mitaa na kata ili kufanya kaguzi mbalimbali za usafi wa mazingira kwenye maeneo yao.
- Uundwaji wa sheria ndogondogo za usafi wa Mazingira zinazotumiwa na CLTS K=katika maeneo yao katika kata saba (7) na Mitaa 38.

- **Ukaguzi wa kiafya katika majengo ya biashara (inspection of premises)**

Ukaguzi wa kiafya umefanyika katika maeneo ya biashara, nyumba za kulala wageni, viwanda, mashine, taasisi na maeneo ya umma. Lengo la ukaguzi huu ni kuhakikisha tunadhibiti ulipukaji wa magonjwa katika jamii na kuhakikisha watoa huduma wanazingatia taratibu zote zilizoainishwa katika sheria ya afya ya jamii NO. 1 ya mwaka 2009 pamoja na kanuni zake za mwaka 2012 na 2018. Jumla ya maeneo ya biashara 1,531 yamekaguliwa pamoja na taasisi 54 Kiasi cha fedha kilichokusanywa katika ukaguzi ni 1,250,000 faini na 1,415,000 fedha ya kupima (medical examination fees).

- **Shughuli za hifadhi na utunzaji wa mazingira**

Halmashauri imesimamia na kufanya shughuli mbalimbali zinazohusu hifadhi ya Mazingira katika kuonyesha jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama ifuatavyo;

i. **Utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji miti milioni 1.5 kila Halmashauri kwa mwaka**

Halmashauri imeendelea kuimarisha hifadhi, utunzaji wa Mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kupitia utekelezaji wa Kampeni ya kitaifa ya Upandaji Miti milioni 1.5 kwa mwaka kwa kila Halmashauri ya Wilaya. Ambapo kupitia mradi wa kitalu cha miti cha Halmashauri katika mwaka wa fedha 2020/2022 Halmashauri ilitenga jumla ya Tsh 10,000,000/= kwa ajili ya uoteshaji wa miche,na miti iliyooteshwa na kugawiwa kwa wananchi na taasisi (shule, hospitali na vyanzo vya maji) mbalimbali ni jumla ya miche 21,680.

ii. **Kusimamia utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kudhibiti utekelezaji wa shughuli yoyote ya kibinadamu inayoweza kuleta athari katika maeneo ya vijito/makorongo kwa kuzingatia mita 60.**

Halmashauri imeendelea kulinda na kuhifadhi vyanzo mbalimbali vya maji vilivyopo kwa kupanda miti na kuzuia shughuli zinazoharibu ikolojia ya maeneo hayo ndani ya mita 60 kutoka fukwe za vyanzo vya maji, vijito/makorongo kama sheria ya usimamizi wa mazingira 2004 inavyoeleza, kwa kutoa elimu hasa kwa wakulima katika kata ya Mpande, Mpemba, Sogea.

iii. **Kufanya Mapitio ya ripoti za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (Environmental Impact Assessment) kwa miradi ya maendeleo.**

Halmashauri imesimamia na kushauri wawekezaji kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira na jamii Katika Miradi ya Ujenzi, kusajili miradi yao kabla ya uwekezaji, kutembelea na kukagua maeneo ya miradi, kupitia na kuhakiki ripoti za tathmini za athari ya Mazingira za miradi mbalimbali kabla kutoa maoni juu ya mradi husika kama sheria ya Mazingira No. 20 ya mwaka 2004 Kifungu cha 81 kinavyoelekeza, ambapo katika mwaka 2021/2022 ilifanya na kufanya mapitio ya ripoti ya Tathimini ya Athari ya Kimazingira na jamii(TAM)-EIA/ESIA) kumi na moja (11) ikijumuisha taasisi za umma na binafsi, sambamba na kuandaa mipango miwili (2) ya usimamizi wa Mazingira na jamii katika miradi ya SEQUIP (Environmental and social management plans-ESMP)

iv. **Elimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

Halmashauri imeendelea kuongeza uelewa kwa jamii juu ya utunzaji na hifadhi ya Mazingira kupitia mikutano ya wananchi kwenye mitaa, vikao mbalimbali kamati za maendeleo ya kata, vikao vya halmashauri ambapo agenda ya usafi na Mazingira kuwa ni agenda ya kudumu,

Kupitia maadhimisho ya siku ya Mazingira duniani ambapo hufanyi kila mwaka 5 juni yakitanguliwa na wiki la maadhimisho hayo kuanzia tarehe 1 -5 juni kila mwaka

**v. Udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi katika Mji**

Kutokana na uwepo wa taka hatarishi kama vile vyuma chakavu, taka za kielekitroniki katika mji, Halmashauri imeanza kuwatambua wadau wanaojihusisha na shughuli za kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha taka hatarishi katika maeneo ya mji kama ambavyo sheria ya usimamizi wa Mazingira 2004 na kanuni zake za udhibiti na usimamizi wa Taka hatarishi za mwaka 2021(The Environmental Management (Hazardous Waste control and management) zinavyoelekeza, ambapo imeweza kuwatambua wadau na vituo kumi na tatu(13) ndani ya Mji(waliopo kata ya mpemba, sogea,majengo, Mpande) wanaojihusisha na ukusanyaji wa vyuma chakavu na mdau 1 aliyepo mtaa wa Tazara kata ya Mpande anayejihusisha na usafirishaji wa taka hatarishi (vyuma chakavu) kuhakikisha kazi hizi zinafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni ili kuimarisha usimamizi wa taka hizi.

- **Kusimamia amri za kudhibiti/kuzuia kelele, mitetemo ya sauti katika maeneo ya biashara (hasa baa na kumbi za starehe)**

Halmashauri imeendelea kusimamia na kudhibiti uchafuzi wa Mazingira utokanao na kelele na mitetemo ya sauti katika baa, kumbi za starehe kuhakikisha na kuwaelekeza wamiliki wa maeneo hayo kuweka vizuia sauti (sound proof) ili kuzuia kelele na mitetemo kutoka nje na kutosumbua wakazi, kulinda afya za binadamu/jamii na mazingira mengine kama sheria ya usimamizi wa mazingira **2004** na kanuni zake za udhibiti viwango vya kelele na mitetemo ya 2015 ambapo kwa Majengo 4 yamekaguliwa.

**Changamoto**

Idara inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli kama ifuatavyo;

- Kuongezeka kwa uzalishaji wa taka ngumu unaotokana na ongezeko la watu na shughuli mbalimbali za kiuchumi
- Kutokuwepo kabisa miundombinu ya mfumo wa maji taka katika Mji
- Kutokuwepo kwa vitendea kazi vya kisasa katika usimamizi wa taka ngumu kama vile sanitary landfill, skip trucks na mitambo mingine ili kuleta ufanisi katika kuondosha taka
- Kutokuwepo na mfumo mzima wa uchambuzi wa taka (sorting), utenganishaji, urejelezaji.
- Uanzishaji wa biashara kiholela usiozingatia matumizi bora ya ardhi mfano gereji, maeneo ya kuoshea magari/pikipiki (car wash)

- Uvamizi wa Maeneo yenye sifa ya kuwa maeneo lindwa kama yalivyotajwa na sheria ya Mazingira no. 20 ya mwaka 2004 kifungu 52.
- Uhaba wa Watumishi wenye fani za Mazingira, misitu

➢ **Mkakati wa uboreshaji wa usafi na hifadhi ya mazingira ya mji**

Mikakati ya kutatua changamoto zilizopo katika idara ni kama ifuatavyo: -

i. Kuanzisha kwa mashindano Usafi wa Mazingira ya kata na mitaa ikiambatana na utolewaji wa zawadi kwa kata na mitaa inayofanya vizuri na adhabu kwa kuonywa
ii. Kutenga bajeti ya ununuzi wa mitambo na vifaa vya kutunzia na kuhifadhia taka, kusafirishia taka hususani skip truck, skip buckets
iii. Kudumisha utekelezaji wa agizo la serikali la kufanya na kutoa hamasa kwa umma juu ya usafi wa mazingira kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi (kama ilivyoelekezwa na Environmental Management-Designation of national Cleanliness Day of 2016) na kila jumamosi ya pili ya mwezi kama ilivyowekwa kwenye mapendekezo ya sheria ndogo ya usafi wa Mazingira ya Mji
iv. Kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika suala la Usafi wanatoa ushirikiano wa uondoshaji wa taka ngumu hasa katika kukandarasi kazi hiyo
v. Kuendelea kuelimisha wananchi na wadau mbalimbali juu ya umuhimu na wajibu wa kila mdau katika kuhakikisha anatunza na kuhifadhi mazingira na kufanya usafi mita tano kuzunguka eneo lake la biashara na Makazi
vi. Kuhuisha na kuandaa kikosi kazi cha vijana ambao watasimamia swala la usafi wa Mji, hususani kufanya ukaguzi wa maeneo yanayo tupiwa taka nje ya utaratibu ulioandaliwa kwa kata zote.
vii. Kuendelea kuandika maandiko ya mradi kwa ajili ya ujenzi wa sanitary landfill kwa ajili kutupia taka
viii. Kushirikisha wadau mbalimbali juu ya upandaji miti katika taasisi na maeneo yao

Kusimamia Tathmini ya Athari za kimazingira na Jamii (EIA/ESIA) katika miradi ya maendeleo ya umma na binafsi.

- **DIVISHENI YA AFYA, USTAWI WA JAMII NA HUDUMA ZA LISHE HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

Halmashauri ya Mji Tunduma katika utekelezaji wa bajeti kupitia Divisheni ya Afya,Ustawi wa Jamii na Huduma za Lishe imetekeleza kama ifuatavyo;-

**Fedha za Ruzuku kutoka Serikali Kuu (OC – Health)**

| NA | Kazi iliyopangwa | Kiasi kilichotolewa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Kuwezesha utoaji wa stahiki mbalimbali za Kisheria kwa Watumishi wa Afya katika Halmashauri ya Mji. | 71,200,000 |
| 2 | Kuwezesha Watumishi wa Idara ya Afya kushiriki Vikao vya Kitaalamu nje ya Halmashauri. | 3,600,000 |
| 3 | Kufanya vikao 2 kwa mwaka kati ya kamati ya Lishe ya wilaya na Wadau wa lishe kutoka asasi zisizo za serikali kwa ajili ya kuboresha mpango kazi mkakati wa lishe kufikia Juni, 2021. | 1,120,000 |
| | **Jumla ndogo** | **75,920,000** |

- **Fedha za mapato ya ndani (Huduma za Lishe)**

| Na | Kazi iliyopangwa | Kiasi kilichotolewa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Kuwezesha utoaji wa elimu ya namna bora ya kuandaa chakula lishe kwenye Mitaa katika Halmashauri ya Mji | 3,360,000 |
| 2 | Kuwezesha stahiki za kisheria Mkuu wa Udara ya Afya. | 12,000,000 |
| 3 | Kuwezesha kufanyika kwa vikao viwili vya tathimini ya hali ya lishe katika jamii za Mji wa Tunduma. | 8,000,000 |
| 4 | Kutoa mafunzo elekezi ya namna bora ya upimaji wa Watoto na uandaji wa lishe bora katika Vituo vya tiba 12 katika Mji wa Tunduma. | 2,800,000 |
| 5 | Kufabya usimamizi shirikishi wa kukaguaa utoaji wa huduma za lishe katika jamii na vituo vya tiba vya Halmashauri ya Mji. | 3,200,000 |
| | **Jumla ndogo** | **29,360,000** |

- **Fedha za wadau wa maendeleo (Afya na Usafi wa Mazingira)**

| Na. | Kazi iliyopangwa | Makisio (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Kuwezesha ukusanyaji wa twakimu za vyoo bora mara mbili kwa mwaka katika Mitaa 71 ya Halmashauri ya Mji Tunduma | 4,320,000 |
| 2 | Kuwezesha kufanyika kwa kampeni ya afya ya usafi na mazingira katika Kata 15 za Miji wa Tunduma. | 3,000,000 |
| 3 | Kufanya tathimini ya Mitaa yenye vyoo bora na kukidhi vigezo vya ODF kwenye mpango wa afya ya usafi na mazingira katika Halmashauri. | 3,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | **10,320,000** |

- **Fedha za wadau wa maendeleo (Shughuli za UKIMWI - WRP)**

| NA | KAZI ILIYOPANGWA | Kiasi kilichotolewa |
|---|---|---|
| 1 | Kuwezesha huduma za kliniki ya CTC kwa Watoto katika vituo vya tiba 5 (Kituo cha Afya Tunduma, Moravian, Holy Family, Zahanati ya Mpande, Chiwezi na Katete) vya Halmashauri ya Mji Tunduma | 21,600,000 |
| 2 | Kuwezesha huduma za upimaji wa virusi vya UKIMWI katika vituo vya tiba 5 (Kituo cha Afya Tunduma, Moravian, Holy Family, Zahanati ya Mpande, Chiwezi na Katete) vya Halmashauri ya Mji Tunduma | 86,000,000 |
| 3 | Kuwezesha utoaji wa elimu ya kijikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika maeneo yaliyoathirika sana na Ugonjwa wa UKIMWI. | 14,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | **121,600,000** |

- **Utekelezaji wa zoezi la Chanjo ya UVIKO-19**

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri imeebdelea kusimamia zoezi la chanjo ya UVIKO-19 na chanzo za Watoto chini ya miaka **5** kama inavyoonesha katika jedwali lifutalo;

| Na. | Kazi iliyopangwa | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. | Kuwezesha utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwa walengwa 91,507 | Jumla ya Wakazi 14,314 wamepata angalau chanjo dozi ya kwanza. Aidha Wakazi 10,293 (Me 6763 Ke 3510) wamekamilisha dozi ya chanjo ya UVIKO -19 sawa na **11.2%** |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Kuwezesha utoaji wa chanjo ya matone kwa Watoto chini ya miaka mitano 29, 606 | Watoto 41944 sawa 114.7% wamepatiwa chanjo ya ugonjwa wa kupooza (Polio). |

**Mhe.Mwenyekiti**

Natoa rai kwa wananchi kujitokeza ili kupatiwa chanjo dhidi ya UVIKO-19 kwani bado ugonjwa huu ni hatari kwa ustawi wa jamii yetu.Hali kadhalika kuwapeleka Watoto kwenye chanjo ili kujikinga maradhi kama vile Polio.

- **TAARIFA YA UTEKELEZAJI ZOEZI LA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTKODI**

**Mhe.Mwenyekiti**

Halmashauri ya Mji wa Tunduma ilifanya uzinduzi wa Mfumo wa anuani za makazi na Postikodi kimkoa tarehe **19/02/2022**. Uzinduzi huu ulifanywa na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Songwe Omary T. Mgumba.Baada ya uzinduzi huo ulitoa nafasi ya kuanza rasmi utekelezaji wa Mfumo wa anuani za makazi na Postikodi

Aidha Halmashauri ya Mji wa Tunduma ilianza zoezi hili kwa kutoa elimu kwa viongozi wa kata (Wah. Madiwani na Watendaji wa Kata), Viongozi wa Mtaa(Watendaji wa Mitaa na wenyeviti), pamoja na mabalozi wote,Viongozi wa dini mbalimbali, viongozi wa vyama vya kisiasa, Wajasiriamali pamoja na vikundi mbalimbali. Elimu hii ilikuwa ni kujenga uelewa wa pamoja ili kufanya zoezi kwa ufanisi zaidi.

Halmashauri ya Mji wa Tunduma ilipokea fedha kiasi cha **shs.91, 832,904.10** kutoka Serikali kuu kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa zoezi la Operesheni ya anuani za makazi kwa ajili ya malipo ya watumishi/Vijana wanaokusanya taarifa za anuani za makazi, kutengeneza nguzo na vibao pamoja na posho za wataalamu wa kuendesha na kusimamia zoezi la anuani za makazi

Halmashauri ya Mji wa Tunduma ilitangaza nafasi za kazi (Wakusanya taarifa za anwani za makazi) na kufanya usaili kwa vijana (**Watumishi 213**) ambao walifanyiwa mafunzo kuanzia tarehe **14/03/2022 hadi 18/03/2022** na kuanzia tarehe **19/03/2022. z**oezi hili liliendelea kwa kuanza kugawa namba za nyumba na kuingiza katika mfumo wa **NAPA (National Physical Address).** Katika zoezi hili watumishi hawa wameweza kukusanya na kuingiza anwani za makazi katika mfumo wa **NAPA.**.

Halmashauri ya Mji wa Tunduma tumetekeleza oparesheni ya anwani za makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**,** Kazi zilizofanywa ni pamoja na;

(a) Kuweka nguzo na vibao kwa ajili ya majina ya Mitaa/Barabara ambapo mirunda **1135** imesimikwa kwa muda kisha itabadilishwa kwa chuma kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa .Aidha TARURA walichangia vibao 65 na walitengeneza vingine 363, Benki ya POSTA wapo kwenye utekelezaji.

(b) Kubandika namba kwenye nyumba.

- **Idadi ya Anwani zilizopaswa kutambuliwa na kusajiliwa 2021/2022**

Katika utekelezaji wa zoezi la anwani za makazi, Halmashauri ya Mji Tunduma ilitakiwa kusajili nyumba 29,983 ambapo hadi tarehe 25/05/2022 saa **3:00** asubuhi idadi ya anwani zilizokuwa zimesajiliwa kwenye mfumo ni 30,008 sawa na asilimia **100.09%**

- **Idadi ya barabara zilizopewa majina 2021/2022**

Lengo ni kufikia barabara **1325** ambapo hadi kufikia tarehe 25/05/2022 jumla ya barabara 1325 zimeingizwa kwenye mfumo ikiwa ni sawa na asilimia 100%.

- **Majengo na viwanja vilivyoainishwa 2021/2022.**

Malengo ya kusajili Majengo na viwanja ni **29,983** ambapo hadi tarehe **25/05/2022** jumla ya majengo na viwanja yamesajiliwa kwenye mfumo ni 30,009 ambapo ni sawa na asilimia **100.09.**

- **Makazi yaliyowekwa vibao (2021/2022) na malengo ya mwaka 2022/2023**

| **na** | **Jina la Halmashauri** | **Malengo** | **Makazi yenye vibao 2021/2022** | **Asilimia** | **Malengo 2022/2023** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tunduma | 29,983 | 29,983 | 100% | Kuweka vibao kwenye makazi 250. | Maandalizi ya uwekaji wa vibao vya plastiki unaendelea kupitia ngazi ya Mitaa na |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Kata ili kuboresha Zaidi. |

Namba za makazi zimeandikwa na kuboresha kwa kuandika namba hizo kwa rangi nyeusi na njano kwa Anwani **29,983**

- **Idadi ya Mitaa/Barabara iliyosimikwa vibao na nguzo 2021/2022.**

| Na | Jina la Halmashauri | Malengo | Mitaa/Barabara zenye nguzo na vibao | Asilimia | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| | Tunduma | 1200 | 1200 | 100% | |

- **Mchanganuo wa takwimu za anwani za makazi kwenye mfumo kwa mwaka 2021/2022 na malengo ya mwaka 2022/2023**

| Na | Halmashauri | Malengo | Anwani kwenye mfumo | Asilimia | Malengo 2022-2023 | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tunduma TC | 29,366 | 30,007 | 100.09% | Kuingiza kwenye mfumo Anwani 250. | |

- **Mchanganuo wa barabara kwenye mfumo 2021/2022 na malengo ya mwaka wa fedha 2022/2023**

| Na | Halmashauri | Malengo | Barabara kwenye mfumo | Asilimia | Malengo 2022/2023 | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tunduma TC | 1300 | 1325 | 101.9% | Kuingiza mtandao wa barabara 25 kwenye mfumo. | |

- **Mchanganuo wa fedha 2021/2022**

**I. Mchanganuo wa matumizi ya fedha za kutoka Serikali kuu**

Halmashauri ya Mji ilipokea kiasi cha Tsh. **91,832,904.01** kutoka Serikali Kuu.Mgawo na matumizi ya fedha kwa Halmashuri ni kama ifuatavyo:

| **Halmashauri** | **Mgao** | **Matumizi** | **Fedha iliyobaki** | **%** |
|---|---|---|---|---|
| Tunduma Tc | **91,832,904.01** | **91,832,904.01** | 0.00 | 100% |

**II. Mchanganuo wa matumizi ya fedha kutoka mapato ya ndani 2021/2022**

| **Halmashauri** | **Fedha tolewa** | **Matumizi** | **Fedha iliyobaki** | **Tumika%** |
|---|---|---|---|---|
| **Tunduma Tc** | **15,000,000.00** | **10,000,000.00** | **5,000,000** | **66%** |

**Changamoto**

1. Mwitikio mdogo wa wananchi juu ya utengenezaji wa vibao na nguzo kwa ajili ya makazi na barabara/mitaa.
2. Changamoto ya mtandao (internet) kuwa chini na muda mwingine kutopatikana kabisa kutokana na matengenezo ya mfumo kila wakati.
3. Mgongano wa majina ya barabara kati ya TARURA na wananchi kwa barabara zilizo sajiliwa na TARURA wananchi hawakuwa tayari kuzipokea.
4. Admini kutokuwa na uwezo wa kuhariri taarifa baada ya kupandishwa taarifa kutoka kwa mkusanya taarifa (Data collector).
5. Baadhi ya maeneo vijijini kutokuwa na mtandao na kufanya wakusanya taarifa kukusanya nje ya mfumo (offline).
6. Mfumo kucheza na kufanya waratibu kushindwa kupata taarifa ya takwimu kwa wakati.

**Utatuzi wa changamoto**

1. Kuendelea kuwaelimisha wananchi umuhimu wa anwani za makazi na postikodi pamoja kuchangia gharama za vibao na nguzo katika makazi na barabara/mitaa yao.
2. Halmashauri imeendelea kuchangia kwenye kutengeneza vibao na nguzo pia kutafuta wadau wanaoweza kufanya kazi hizo kama vile TARURA wametoa na kusimika vibao 426 vya chuma. Halmashauri

3. Wakusanya taarifa hukusanya nje ya mtandao (offline) na baadaye kukusanyika maeneo yenye mtandao na kutuma taarifa baada ya muda wa kazi nyakati za jioni au usiku
4. Tumewashauri Tarura kusikiliza matakwa ya wananchi kutoa majina Barabara walizo kubaliana kutokana na vikao vyao.

**Pendekezo la uchangiaji wa kiasi cha Tshs 2000 kwa ajili ya utengenezaji wa vibao vya namba za nyumba.**

Baada ya wasilisho la pendekezo la kiwango cha Tshs **2000** kwa ajili ya uchangiaji wa utengenezaji wa vibao vya nyumba kuidhinishwa na Kikao cha Kamati ya Fedha, Halmashauri kwa kushirikiana na viongozi wa Mitaa na Kata inatarajia kuratibu zoezi la uwekaji wa vibao hivyo kwa kila nyumba sambamba na kurekebisha maeneo ambayo hayakuweza kufikiwa wakati wa zoezi la awali kutokana na changamoto zilizoainishwa hapo juu.

**Malengo na utekelezaji wa zoezi la anwani za makazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

Halmashauri imetenga kiasi cha Tshs. **20,000,000/=** kwa mapato ya ndani katika utekelezaji wa zoezi la Anwani za Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

| Na | Halmashauri | Malengo | Muda wa utelekezaji | Asilimia | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Tunduma | Kuingiza Anwani 250 kwenye mfumo. | Robo I, Robo II, Robo III. | | Utekelezaji utaanza baada ya kufunguliwa kwa mfumo wa malipo Fedha. |
| | | Kusimika vibao na nguzo 400. vya chuma. | Robo I, Robo II, Robo III. | | Utekelezaji utaanza baada ya kufunguliwa kwa mfumo wa malipo Fedha. |
| | | Kuweka vibao kwenye | Robo I, Robo II, Robo III. | | Utekelezaji utaanza baada ya kufunguliwa kwa mfumo wa malipo Fedha. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | makazi 250. | | | |
| | | Kuingiza mtandao wa barabara 25 kwenye Mfumo. | Robo I, Robo II. | | Utekelezaji utaanza baada ya kufunguliwa kwa mfumo wa malipo Fedha. |

- **MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2022**

**Mhe.Mwenyekiti**

Mbio za Mwenge wa Uhuru **2022** zilizinduliwa Kitaifa Mkoani Njombe mnamo tarehe **01.04.2022** na utazimwa Mkoani Kagera mnamo tarehe **14.10.2022.** katika maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Vijana.

Aidha katika Mkoa wa Songwe Mwenge utapokelewa kutoka Mkoa wa Mbeya tarehe **14.09.2022** na kukimbizwa mfululizo katika Halmashauri zote tano (5).

Katika Halmashauri ya Mji Tunduma Mwenge wa Uhuru utapokelewa katika Mtaa wa Nandanga Kata ya Mpemba mnamo tarehe **17.09.2022** ukitokea Wilaya ya Ileje.

**Mhe.Mwenyekiti**

Mwenge wa Uhuru ukiwa katika Halmashauri ya Mji Tunduma utazindua,utaweka Mawe ya msingi na kukagua jumla ya miradi **06** na shughuli za vikundi vitatu (**03)**. Miradi pendekezwa inakadiriwa na thamani ya Shs**. 2,378,000,000.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali.

**Mhe.Mwenyekiti**

Maandalizi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru **2022** yanafanywa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Momba kupitia Kamati iliyoundwa ambapoi tayari vikao vinafanyika kama ilivyopangwa sanjari na kuhimiza michango kutoka kwa wadau mbalimbali. Aidha timu maalum ya Wataalam iliyoundwa inafanya ufuatiliaji na kukagua nyaraka katika miradi itakayopitiwa na Mwenge wa Uhuru **20202.**

**Mhe Mwenyekiti**

Natoa rai kwa Waheshimiwa Madiwani, wananchi na wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu na kutoa ushirikiano katika kufanikisha Mapokezi na hata Mkesha wa Mwenge katika Viwanja vya Shule ya Msingi Tunduma iliyopo Kata ya Uwanjani.

**HITIMISHO**

**Mhe.Mwenyekiti**

Ninatoa shukrani za dhati kwa Baraza lako Tukufu, Timu ya Menejimenti na wananchi kwa ujumla kwa ushiriki wao chanya katika mafanikio yalipatikana katika mwaka **2021/2022** kwenye nyanja mbalimbali kama vile ukusanyaji wa mapato,usafi wa mazingira,chanzo dhidi ya UVIKO-19,usimamizi wa miradi ya maendeleo na matokeo mazuri ya mitihani ya Kitaifa.

Kipekee ninatoa shukrani za dhati kwa Mhe.Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.David Ernest Silinde (Mb) Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala na Serikali za Mitaa, Waheshimiwa Wabunge Viti Maalum Mkoa wa Songwe, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mkuu wa Wilaya ya Momba na Viongozi mbalimbali katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayosisitiza katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Shime tujitokeze katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika tarehe **23** Agosti **2022.**

**Mhe.Mwenyekiti,**

**Naomba kuwasilisha,**

Philemon M.Magesa

**MKURUGENZI**

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**